# Nipashe

Jumatatu Oktoba 7, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580042

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

ashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



## Wanafunzi nane mbaroni tuhuma mauaji mwenzao

UKURASA 2


HABARI ZANZIBAR

Nipashe 23

UWT waambiwa wabadilike

Walimu waahidiwa kuendelea kusoma

Apongeza wananchi kushirikiana na SMZ

UKURASA 23

# Magufuli awaweka pagumu watumishi

• **Awataka** watekeleze au wafukuzwe kazi • **Aagiza** kigogo Polisi kusimamishwa kisa... *Endelea ukurasa 2*




Rais John Magufuli akizungumza na askari wa Jeshi la Polisi wakati akielekea kukagua Kituo cha Polisi cha Laela mkoani Rukwa, baada ya kufungua barabara ya Tunduma-Sumbawanga, jana. **PICHA: IKULU**

## Wanunuzi tanzanite waibua mapya

UKURASA 8

## Mbunge ajitokeza kumrithi Mbowe uenyekiti Chadema

UKURASA 2

**MICHEZO** **MIRAJI ATOA SIRI YA TUZO SIMBA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Wanafunzi wanane mbaroni tuhuma mauaji mwenzao

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI wanane wa Sekondari ya Seeke mkoani Shinyanga, wanashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumshambulia na kusababisha kifo cha mwenzao.

Mwanafunzi aliyeshambuliwa na baadaye kupoteza maisha ni Constantine Makoye (18), aliyepata majeraha makubwa yaliyosababisha kupoteza maisha wakati wa matibabu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa, Richard Abwao, alisema shambulio hilo lilitokea Oktoba 29, saa 12 jioni, katika Kanisa la Wasabato ambako kulikuwa na sherehe ya kuwaaga wanafunzi washirika wa kanisa hilo wanaotarajia kuhitimu kidato cha nne mwezi ujao.

Alisema ugomvi ulitokea siku hiyo, uliibuka baada ya kundi la wanafunzi wakiongozwa na Isaya Athuman (18) wa kidato cha nne na wenzake 10 ambao hawakualikwa kwenye sherehe hiyo, walimvamia Makoye na kuanza kumpiga.

Abwao aliwataja vijana hao kuwa ni Isaya Athuman (18), Godfrey Simon (18), Enock Boniface (18) pamoja na Emmanule Sekela (18) na wengine wanne majina tunayo kwa vile hawajafikia miaka 18, wote wa Sekondari ya Seeke.

Aidha, alisema baada ya kumvamia walimshambulia huku wakimnyang'anya viatu na maji ya kunywa.

Alisema wanafunzi hao walipiga kelele na mayowe kuomba msaada kuwa wamevamiwa na kuanza kuwarushia mawe waliovamia hao.

"Baada ya kurushiwa mawe wavamizi hao walikimbia na kutawanyika, lakini Constantine Makoye alizidiwa akiwa amelala chini na wenzake walimtelekeza hadi alipopata nguvu na kwenda nyumbani kumjulisha babu yake ambaye alimpeleka kutibiwa katika hospitali bila kutoa taarifa polisi," alisema Abwao.

Alisema ilipofika Jumanne wiki iliyopita Makoye alikuwa hawezi kuongea, ndugu zake walitoa taarifa kituoni poleni na kufungua jalada la kulalamikia kujeruhiwa kabla ya mwanafunzi kufariki Oktoba 2, katika Hospitali ya Mji wa Kahama.

Kamanda alisema chanzo cha kifo chake ni majeraha makubwa kichwani na kwamba mwili wake umekabidhiwa kwa ndugu zake kwa taratibu za mazishi.

# Magufuli awaweka pagumu watumishi

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli jana, aliwabana watumishi wa umma na kutoa siku kadhaa kwa wanaokalia majengo binafsi kuhamia kwenye majengo ya serikali na atakayeshindwa kutekeleza hivyo afukuzwe kazi.

Akizungumza jana na wananchi wakati wa uzinduzi wa barabara ya Tunduma hadi Sumbawanga yenye Km 223.1, Mji mdogo wa Laela mkoani Rukwa, alisema majengo ya serikali yapo lakini taasisi na mashirika ya serikali wamepanga kwenye majengo binafsi.

Aidha, alitoa maelekezo kwa kila taasisi na mashirika kuondoka kwenye majengo hayo na kuhamia kwenye majengo ya serikali, huku akieleza kuwa kwamba ambao wataendelea kubaki kuwe na sababu za msingi zitakazomridhisha.

**AIPA TANROADS SIKU 5**

Rais aliagiza Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), kuhama kwenye ofisi za jengo walilopanga ndani ya siku tano.

Alisema Tanroads wanalipa Sh. bilioni 2 kila mwaka, licha ya kuwa taasisi ya muda mrefu huku Wakala wa Barabara Vijijini (Tarura), iliyoanza miaka ya karibuni wameshajenga jengo lao jijini Dodoma, huku wenzao wamepangisha.

"Ndani ya siku tano nakupa Patrick Mfugale ukawaambie watu wako wahamie kwenye majengo ya serikali," alisisitiza.

Aidha, alisema anatoa ujumbe kwa taasisi na mashirika ya umma yaliyopanga kwa malengo ya kupata asilimia (rushwa), huku akiwapa mwezi mmoja wahamie kwenye majengo ya serikali.

**HALMASHAURI YAPEWA MWEZI MMOJA**

Alisema amesikitishwa na watendaji wa Halmashauri ya Sumbawanga Vijijini kuendelea kukaa mjini kwenye majengo ya Manispaa ndani ya eneo la mita 200.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, ilivyoanzishwa hHlmashauri ya Sumbawanga Vijijini lengo ni kusogeza huduma kwa wananchi, lakini hadi sasa hawajahama.

"Mkurugenzi akitaka kuwahudumia wananchi anatembea kilomita 95 kwenda na kurudi, ofisa kilimo, mifugo. Nataka Halmashauri ya Sumbawanga Vijiiji mhame haraka na kuhamia Laela, anayetaka ukurugenzi ahamie hapo, hatuwezi kwenda kwa michezo ya...namna hii, kama ilianzishwa halmashauri, meya na mkurugenzi wanakaa mjini tuliianzisha ya nini," alisema.

Aidha, alitoa mwezi mmoja na kwamba anayetaka kazi aende akakae katika eneo hilo, huku akiagiza magari yote ya halmashauri kwenda eneo hilo.

"Tumedekezana mno, ikiwa ofisi ya wilaya imeanzishiwa hapa nyie mnasubiri nini? Waziri Jafo ninataka hao watendaji wako waje hapa, ambaye hataki anataka kukaa mjini fukuza moja kwa moja," alisema.

INAENDELEA UK.26



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiangalia mbegu za pamba katika kiwanda cha kuchambulia pamba cha Biosustain, wakati alipotembelea kiwanda hicho kilichopo Mandewa katika Manispaa ya Singida, jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho, Dk. Riyaz Haider. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mbunge ajitokeza kumrithi Mbowe uenyekiti Chadema

**Na Enock Charles**

VUGUVUGU la uchaguzi ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), limeanza baada ya Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe, kutangaza nia ya kutaka kuwa mrithi wa Freeman Mbowe.

Kwa sasa chama hicho Mwenyekiti wake ni Mbowe, na kwa mujibu wa Katiba yao wanatakiwa kufanya uchaguzi wa ndani ya chama.

Hivi karibuni, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilikitaka Chadema kuwasilisha maelezo katika ofisi yake kwa kile alichoeleza ni kukiukwa kwa Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kusogeza mbele uchaguzi wa viongozi wake.

Katika barua hiyo Msajili iliagiza maelezo hayo kuhusu sababu za kuahirishwa kwa uchaguzi huo kuwasilishwa katika ofisi hiyo kufikia Oktoba 7, mwaka huu (leo) saa tisa na nusu mchana. Akizungumza na gazeti hili kuhusiana na nia yake ya kukiongoza chama hicho kikuu cha upinzani nchini, Mbunge huyo, alisema umefika wakati kwa chama hicho kupata mwenyekiti mpya, kwamba ameamua kugombea nafasi hiyo kwa kile alichodai kuwa na sifa za kuongoza.

"Tunamshukuru Mwenyekiti wetu kwa mambo mengi mazuri aliyokifanyia chama chetu na imefika wakati sasa kuwaachia wengine," alisema Mwambe.

Mbunge huyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama hicho Kanda ya Kusini na mjumbe wa Kamati Kuu, alidai kuwa na uwezo wa kuongoza chama hicho baada ya kupata uzoefu wa kuongoza ukanda huo, hivyo sasa anaona anatosha kwa nafasi ya taifa ndani ya chama hicho.

Hivi karibuni, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, alisema uchaguzi wa viongozi wa chama hicho kwa ngazi ya kitaifa unatarajiwa kufanyika Desemba mwaka huu.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji, wiki iliyopita, alinukuliwa akisema kulikuwapo na sababu kadhaa zilizosababisha uchaguzi wa viongozi wa chama hicho kuchelewa na kufafanua kuwa utafanyika kabla ya kumalizika mwaka huu.

Dk. Mashinji alikuwa anatoa ufafanuzi kuhusiana na barua ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.



Makamishna wa Polisi wakiongozwa na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz (katikati) na kulia Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Liberatus Sabas, Kamishna wa Kamisheni ya Polisi Maabara na Uchunguzi wa Kisayansi, Shaban Hiki na kushoto kwa Boaz ni Kamishna wa Kamisheni ya Polisi Intelijensia ya Jinai, Charles Mkumbo, wakiwa na wahandisi wa ujenzi wa mradi wa umeme Rufiji baada ya kufanya ziara ya siku moja. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Majaliwa acharuka ujenzi kituo afya

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema hajaridhishwa na ujenzi wa kituo cha afya cha Ndago, wilayani Iramba mkoani Singida kwa sababu uko chini ya kiwango.

Alitoa kauli hiyo jana, wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Ndago, baada ya kukagua majengo ya kituo hicho.

"Nimepita kote nchini kukagua vituo hivi, lakini hapa wamenikasirisha. Wameniletea kwenye jengo nilikague nikajua ni jipya kumbe ni la zamani. Lazima nikiri kwamba fedha yetu hapa haijakamilika, jengo la mama na mtoto halijakamilika. Nilipouliza linakamilika lini, wananijibu tuko kwenye final touches (tuko hatua za mwisho)," alisema. "Jengo lile halivutii kabisa, wanaotoa maelezo hakuna kinachoeleweka. Sijaridhishwa kabisa na hali hii. Jengo la upasuaji nalo pia nimeona ni la zamani. Hii ina maana hamjajenga jengo jipya. Mimi nataka nione jengo jipya hapa," alisisitiza.

Alipomuuliza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Leno Mwageni, amebakiza kiasi gani cha fedha katika Sh. milioni 400 ambazo ziliitwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo, Mkurugenzi huyo alijibu kwamba hakuna kiasi cha fedha kilichobakia.

Waziri Mkuu aliwaeleza wananchi hao kwamba Rais John Magufuli anatambua wao hawana uwezo, na tena wanaugua na kuna watu ambao wanapoteza maisha kwa sababu hawawezi kufika kwenye tiba kwa wakati. "Vituo vya afya vinajengwa kila mahali nchini ili wewe mwananchi usilipe nauli kwenda Iramba Mjini au Singida Mjini kutafuta tiba, bali upate vipimo vyote hapa hapa ulipo. Vipimo vya magonjwa yote vinapatikana hapa hapa."

"Fedha hizi zikiletwa zinataka zijengwe maabara, chumba cha upasuaji mdogo na mkubwa, chumba cha huduma ya mama na mtoto, chumba cha kuhifadhia maiti na nyumba ya mkuu wa kituo, lakini hapa Ndago fedha yetu imeharibika," alisema.

Alipoenda kukagua chumba cha kuhifadhia maiti, Waziri Mkuu alikuta limewekwa mlango wa mbele tu na vyumba vingine vyote havina milango wala mabomba na masinki hayajakamilika tofauti na taarifa aliyopewa kwamba jengo hilo liko tayari.

"Mkurugenzi nimekuta wagonjwa wamelazwa katika baadhi ya vyumba na kazi haijakamilika. Huwezi kupanga vifaa wakati ujenzi unaoendelea ili kumdanganya Waziri Mkuu. Na wala hunidanganyi mimi bali unawadanganya wananchi."

"Ninazo taarifa kwamba jana mlikesha kupanga vitu ndani. Nenda kaondoe vifaa vyote hadi ujenzi utakapokamilika ndipo madaktari warudi kuendelea na kazi. Serikali hii haiwezi kuvumilia vitu vya ovyo. Hatua kali zitachukuliwa," alisisitiza.

# Hatima ya Wambura leo

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya Makamu wa Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura, kuhukumiwa au la itajulikana leo baada ya Ijumaa iliyopita kurudishwa mahabusu na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kupanga kusikiliza leo maombi yake ya kumwandikia barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) kuomba msamaha na kukiri makosa yake.

Wambura ambaye anakabiliwa na mashtaka ya kughushi na kutakatisha fedha, alifikishwa mahakamani hapo Ijumaa mchana baada ya wito wa mahakama.

Mahamama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kevini Mhina, ilipiga kalenda kesi hiyo mpaka leo baada ya Wambura kudai kuwa kwa mujibu wa makubaliano yake ana uwezo wa kulipa faini ya Sh. milioni 85 na si Sh. milioni 100.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alidai kuwa bado hajajiandaa na mahakama hiyo imepanga kusikiliza maombi yake leo.

Awali katika kesi hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika aliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Wambura alinyoosha mkono kuomba kuongea, mahakama ilimruhusu.

"Mheshimiwa hakimu nimemwandikia barua DPP kuomba msamaha na kukiri makosa yangu, naomba Jamhuri waharakishe nipate majibu ya barua yangu," alidai Wambura.

Wankyo alidai kuwa amesikia hoja za mshtakiwa na kwamba atafuatilia na kuzifanyia kazi.

Hakimu Mhina alisema kesi hiyo itatajwa Oktoba 16, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi kigogo huyo wa mpira wa miguu nchini, anakabiliwa na mashtaka 17, likiwamo la kughushi, shtaka moja la kutoa na kuwasilisha nyaraka za uongo; mashtaka 13 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na mashtaka mawili ya kutakatisha fedha haramu.

# Anayedaiwa kumbaka bintiye hukumu Ijumaa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha imepanga kutoa hukumu Oktoba 11, mwaka huu, dhidi ya kigogo wa Taasisi ya Utafiti na Udhibiti wa Viuatilifu katika ukanda wa Kitropikali ya (TPRI), Aresteric Silayo, anayedaiwa kumbaka mwanawe wa kike (11).

Akizungumza mahakamani hapo juzi, Hakimu Mkazi Aziza Temu, aliyepewa mamlaka na Mahakama Kuu Kanda ya Arusha kusikiliza rufani ya kesi hiyo, alisema amesikiliza hoja za rufani hiyo za pande zote mbili.

"Baada ya kuwasikiliza upande wa utetezi na Jamuhuri, hukumu nitatoa Oktoba 11, mwaka huu," alisema.

Kabla ya hakimu Aziza kupanga tarehe hiyo, alimsikiliza Wakili wa Serikali, Azael Mwiteni, ambaye aliomba mahakama hiyo kutengua uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha ya kumwachia huru mtuhumiwa huyo.

"Mheshimiwa naomba utengue uamuzi wa kumwachia huru mtuhumiwa huyu na kuzingatia ushahidi wa mtoto na mashahidi wote waliofika mahakamani hapa kutoa ushahidi unaofanana na usio na mashaka," aliiambia mahakama.

Alieleza ushahidi wa mtoto (jina tunalo) unaonyesha baba (mtuhumiwa) alimbaka mwanawe kwani mtoto aliweza kumweleza Mwalimu shuleni, mahakamani na pia cheti cha daktari aliyemchunguza amethibitisha mtoto huyo kubakwa.


## TARIME DISTRICT COUNCIL

**QUOTATION NO. LGA/067/2019/2020/G/01**

**INVITATION FOR QUOTATIONS**

**Date 7/10/2019**

1. Tarime District Council set a funds for the **Supply of Smart Point of Sale (Pos) at Tarime District Council.**
2. During the financial year **2019/2020** It is intended that part of the proceeds of the fund will be used to cover eligible payment under the contract for which this invitation for quotation is issued.
3. Tarime District Council inviting qualified suppliers their price quotation for executing the works as described in the Bills of Quantities (BOQs) as shown in **Section II**
4. All quotations in one original plus two copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes marked **Quotation No. LGA/067/2019/2020/G/01** must be delivered to the address tender Board Secretary, **Tarime District Council P.O Box 16 Tarime.**
5. The deadline for submission of quotations is **12:00 hour's** local time on **Thursday 10/10/2019** Quotations will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderer's representatives who choose to attend in the opening at the **Tarime District Council Head Quarter**
6. Late quotations, portion of quotations, electronic quotations, quotations not received, quotations not opened at the quotation opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**Apoo C. Tindwa**
**District Executive Director**
**TARIME**

215447702

# Bonite Bottlers yazindua promosheni ya zawadi

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya vinywaji baridi ya Bonite Bottlers imezindua promosheni itakayo wawezesha wateja wake kujishindia zawadi mbalimbali.

Baadhi ya zawadi hizo ni bodaboda, televisheni na katoni za maji ya kunywa ya Kilimanjaro.

Kampuni hiyo ambayo huzalisha vinywaji baridi vya jamii ya Coca-Cola ikiwamo soda za Coca-Cola na maji ya kunywa ya Kilimanjaro imetoa rai kwa wateja wake kuchangamkia promosheni hiyo itakayohusisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa promosheni hiyo jijini Dar es Salaam juzi, Mkuu wa Masoko na Mauzo wa Kampuni ya Bonite, Christopher Loiruki, alisema promosheni hiyo itadumu kwa miezi miwili ambapo itaanza rasmi Oktoba 7 na

INAENDELEA UK. 26



Meneja wa Masoko na Mauzo wa Bonite Bottlers, Christopher Loiruk, akizungumza na waandishi wa habari katika uzinduzi wa promosheni ya maji ya Kilimanjaro ambayo inaanza leo na itawawezesha wateja wake wa jumla kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo bodaboda na televisheni na zawadi ya katoni za maji hayo. Mkutano huo ulifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Yasini Hussein na Shafiul Rahmani ambaye ni Meneja Mauzo. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Watumishi 48 kuchunguzwa ubadhirifu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Singida, Adili Elinipenda, achunguze watumishi 48 waliojihusisha na upotevu wa fedha kwa njia za udanganyifu.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na madiwani na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwenye mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa halmashauri hiyo.

Alitaja maeneo saba ambayo ametaka yafanyiwe uchunguzi wa kina ili kubaini upotevu huo. Eneo la kwanza ni upotevu wa makusanyo ya ndani kupitia mawakala wa ukusanyaji mapato (POS) ambapo mawakala wanaokusanya fedha wanashirikiana na watumishi wa halmashauri na kuzitumia bila kuziingiza benki.

"Kuna kundi la watumishi 10 wakiongozwa na mtu wa Tehama, wameshirikiana kupata 'password' na fedha zikishakusanywa wanazitoa na kuzitumia bila kuzipelekea benki. Wamesahau kwamba malipo yalipoingizwa mara ya kwanza, data ilirekodiwa kwenye mfumo wa malipo na sisi tunaona ni kiasi gani kimekusanywa."

Watumishi hao ni Salum Omari (Mtaalamu wa Tehama); Adam Mzengi (Mhasibu kahamishiwa Gairo); Rafaeli Nasari; Caroline Makundi (kahamishiwa Singida Manispaa), Edson S. Ally (Ofisa Biashara); Martin Kimisho (Mhasibu Msaidizi); Prosper Banzi (Ofisa Biashara); Hassan Ponda (Mhasibu kituo cha afya Ndago); Hafidh Ngayunda (Kaimu Mweka Hazina wa Wilaya) na Muhidin Mohammed (Mweka Hazina wa Wilaya) ambaye tayari amesimamishwa kazi kutokana na tuhuma hizo.

Kutokana na upotevu huo, Waziri Mkuu ameagiza Kaimu Mweka Hazina wa Wilaya akae pembeni hadi uchunguzi wa Takukuru utakapokamilika.

Akibainisha mchezo mwingine uliochezwa na watumishi wa Halmashauri hiyo, Waziri Mkuu amesema kuna watumishi 38 ambao walilipwa kiasi cha Sh. milioni 46 ambazo zilikuwa sehemu ya Sh. milioni 400 za kujenga vituo vya afya vya Ndago na Kinampanda wilayani humo.

"Hapa nina vocha zote za malipo walipeana fedha watu hawa akiwamo mkurugenzi wao. Lakini ni kazi gani ambayo kundi lote hili lilikuwa likiisimamia na kustahili kupata malipo hayo? Kutoka makao makuu ya wilaya hadi Ndago au Kinampanda kuna umbali gani?" Alihoji Waziri Mkuu.

"Kamanda wa Takukuru fanya uchunguzi, fuatilia wote waliohusika sababu majina tunayo, kama hawastahili kulipwa ni lazima warudishe fedha yetu. Hii ni sehemu ya Sh. milioni 90 ambazo hazijulikani ziliko na zilikuja kujenga kituo cha afya. Fedha hizi zimekuja na maelekezo rasmi, ni kwa nini zilibadilishwa matumizi?" Alihoji.




# Wanaoandalia watoto wao anguko lawamani

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema baadhi ya Watanzania wanawaandalia watoto wao anguko mbele ya safari kwa sababu hawataki washiriki stadi za kazi shuleni.

Kamishna wa Elimu wa wizara hiyo, Dk. Lyabwene Mtahabwa, aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa viongozi wa wizara na wahariri wa vyombo vya habari na waandishi.

Dk. Mtahabwa wakati akichangia swali lililoulizwa na mmoja wa washiriki wa mkutano huo kuhusu somo la stadi za kazi, alisema shule za sekondari alizozitembelea, wakuu wake wanalalamika kuwa baadhi ya wazazi hawataki watoto wao wapige deki, wafagie, kufua au kulima.

"Ninawasihi sana wahariri na waandishi wa habari nendeni mkawaambie Watanzania wasiwaandalie watoto wao anguko mbele ya safari. Stadi za kupambana na maisha kwa kushiriki mambo mbalimbali ndiyo njia ya kumwandaa mtoto, lini umewahi kuona mtumwa amepanda farasi wa mfalme na mfalme anatembea juu ya nchi kama mtumwa, maana yake maisha ya baadaye hatuwezi kuyatabiri yatakuwaje," alisema.

Dk. Mtahagwa alisema mzazi anayemzuia mtoto wake leo asikamate jembe shule, kesho atalazimika kulikamata hivyo wanafunzi wapewe nafasi ya kushiriki kwenye shughuli zitazowajenga kwa ajili kuwaandaa baadaye kujitegemea.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo, alisema mitaala ya elimu haifundishi watoto kutokuwa na nidhamu wala tabia mbaya.

"Mwanafunzi akiwa kwenye daladala akimwona mtu mzima anajidai amelala lakini akiwa mazingira ya shule anampisha mwalimu, somo la stadi za kazi lipo na wakifanya mitihani wanafaulu, lakini wakifika nyumbani wanayoyafanya ni tofauti," alisema.

Pia alisema watoto wengi wanaopata shida ni wa watu wazito ambao wanaishi maisha ambayo siyo ya uhalisia hivyo baadaye wanapata maanguko na kujiingiza kwenye dawa za kulevya.

# Chanzo magari kuwaka moto safarini chaelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limetoa elimu kwa wananchi kuhusu vyanzo vya magari kuwaka moto yawapo safarini na jinsi ya kujiepusha na majanga hayo.

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Elnimo Shang'a, alisema kuwa chanzo kikuu cha moto kwenye magari ni mifumo ya moto kutohakikiwa kabla na wakati wa safari.

Aliitaja mifumo hiyo kuwa ni pamoja na injini, betri na mfumo unaotoa mafuta kwenye tangi la gari kwenda kwenye injini ya gari. Hivyo, aliwasihi kuhakikisha kuwa pamoja na kuwa makini kuhakikisha mifumo hiyo haina tatizo na haiingiliwi wanapaswa pia kuhakikisha wana vizimia moto (fire extinguishers) vilivyokaguliwa, vinavyotunzwa kwa umakini pamoja na kuwa na elimu ya kuvitumia kwa ufasaha.

"Hivi vizimia moto ambavyo huwa viko kwenye magari vinatakiwa kufanyiwa 'service' angalau mara moja kila mwaka. Lakini mara nyingi sisi huwa tunafanya ukaguzi, lakini mara nyingi hawa wanaovibeba wanavibeba kwa ajili ya kukwepa faini ya polisi wa usalama barabarani na sio kwa sababu ya usalama wa chombo chake," alisema Shang'a wakati akizungumza katika kipindi cha On The Bench kilichoandaliwa na Dar24 Media, ambacho hufanyika mtaani kwa kuwakutanisha wataalamu, viongozi na wananchi wa kawaida,

Ofisa huyo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji aliongeza kuwa kwa sasa Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani kimeshirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, hivyo hata askari wa usalama barabarani wanaweza kufanya ukaguzi wa kizimia moto kama kina ubora na kinaweza kufanya kazi ipasavyo.

Aidha, aliwaelimisha madereva waliokuwa wamekusanyika pamoja na wananchi wengine kuhusu vizimia moto ikiwa ni pamoja na aina zake na jinsi vinavyotumika.

Katika hatua nyingi, Bruno Ndege, mwalimu na mmiliki wa chuo cha ufundi wa magari cha Bruno VTC Buguruni Malapa, jijini Dar es Salaam, aliyekuwa katika kipindi hicho, alitoa ufafanuzi wa vyanzo vya moto kwenye magari yawapo safarini.

Akizungumzia magari makubwa hasa yanayosafirisha mafuta, ambayo yameripotiwa mara nyingi kuteketea kwa moto, alisema yamekuwa katika hatari zaidi kwani yanatumia betri mbili zenye uwezo mkubwa wa moto. Hivyo, kwa kuwa chanzo kikuu cha moto kwenye magari ni betri, zisipowekwa katika hali ya usalama zaidi kwenye magari hayo inakuwa hatari zaidi.

"Hakikisha kitu cha kwanza unakagua, terminal betri zile ziko sawasawa? Je, zile terminal zimefungwa vizuri na spana? Na ukishazikagua ukazikuta ziko sawa unafungua gari lako kwenye boneti au kwenye kibini unaangalia zile nyaya ambazo zimefungwa kwenye starter motor, kuna nyaya zingine zimefungwa kwenye alternator kusiwapo na viungio vilivyolegea," alisema Mwalimu Ndege.

"Kuna magari mengine yanawaka moto yakiwa yanatembea kama hivi unasikia gari limewaka moto. Hizo husababishwa na betri, mfumo wa nyaya na chaji vinapokuwa vimelegea. Kwa hiyo, dereva unapokuwa makini kukagua vile vitu utakuwa umevidhibiti."

"Unapowasha gari, injini inapoanza kufanya kazi moja kwa moja alternator inaanza kuzalisha umeme. Na alternator haiwezi ikapata umeme bila betri. Sasa betri ikishapata umeme ukaingia kwenye alternator ili ianze kuzichaji betri. Ikiwa kuna 'loose connection' kwenye betri na zikawa zinatoka cheche kuna mawasiliano kama kuna tangi lenye leakage ndogo tu, cheche zile zinaweza kusababisha tangi likaripuka kama lina mafuta hata bila gari kuanguka," aliongeza.

Mwalimu Ndege na Ofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji waliwasihi madereva na watu wanaomiliki magari kuepuka kununua vipuri visivyo na ubora kwani vinahatarisha usalama wa gari na vinaweza kuwa chanzo cha gari kuwaka moto.

Waliwataka watumiaji wa magari kutokubaliana na kinachodaiwa mitaani kuwa gari linaposafiri sana wakati wa jua hupata joto na huweza kusababisha kushika moto kuliko linapoendeshwa usiku.

## Sababu madaktari kupewa elimu mionzi

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Aga Khan imeamua kutumia Wiki ya Teknolojia ya Mionzi ya Nyuklia kutoa elimu kwa madaktari baada ya kubaini walio wengi bado wana hofu kuwa mashine zinatumika kuchunguza magonjwa mbalimbali zitawasababishia madhara.

Mkurugenzi wa Tiba kutoka hospitalini hapo, Dk. Ahmed Jusabani, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho hayo ambayo kila mwaka huadhimishwa kuanzia jana.

Alisema huduma hiyo ya mionzi ya nyuklia kufanya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali kama ya tezi dume, saratani, moyo, ini, figo, kichwa, uvimbe kwenye koo na mfumo wa chakula.

Dk. Jusabani alisema teknolojia hiyo ya mashine ya mionzi ya nyuklia hapa Tanzania ipo kwenye hospitali tatu ambazo ni Aga Khan, Ocean Road na Bugando.

"Changamoto iliyopo ni elimu ndogo kwa madaktari na wananchi kuhusu huduma ya nyuklia na faida zake, kupitia wiki ya teknolojia ya nyuklia inayoadhimishwa kila mwaka kuanzia Oktoba 6 (jana) tutaitumia kuwaelimisha na kujua faida ya kipimo na kutokuwa na hofu ya

INAENDELEA UK. 26


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

TRA

## TAARIFA KWA UMMA

Mnamo tarehe 14 Juni, 2018, Waziri wa Fedha na Mipango alitangaza msamaha maalum wa riba na adhabu kwa Walipakodi wenye malimbikizo ya madeni, na wale ambao wako tayari kuweka wazi madeni ya nyuma kwa hiari yao wenyewe na kulipa kodi ya msingi kwa utaratibu ulioanishwa katika (Amri Na. 282A ya Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018.

Mpango maalum wa msamaha wa riba na adhabu ni fursa maalumu ya muda mfupi iliyotolewa. Utaratibu huu ulianza 01 Julai, 2018 hadi Juni 30, 2019 na ilihusisha malimbikizo ya madeni ya kodi yaliyokuwepo.

Hata hivyo, Serikali kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu), (Nyongeza ya muda wa kulipa)2019 , iliongeza muda wa malipo ya kodi ya msingi kufikia tarehe 31 Disemba 2019 kwa walipakodi ambao;

a) waliomba msamaha wa riba na adhabu za kodi kwa Kamishna Mkuu;
b) waliopatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi;
c) waliingia makubaliano na Kamishna Mkuu ya kusamehewa riba na adhabu za kodi kama ilivyoanishwa katika Amri Na. 282A ya Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018;
d) walianza kulipa kodi ya msingi kwa mkupuo au kwa awamu; na
e) mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2019 walishindwa kulipa kiasi cha kodi ya msingi kilichokubaliwa kwa ukamilifu.

Hivyo, wastahiki wote wa msamaha waliopatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi mnakumbushwa kulipa kodi ya msingi kama ilivyoainishwa kwenye mikataba ya makubaliano wa malipo kabla au kufikia tarehe 31 Disemba, 2019 na kwamba hakuna nyongeza zaidi ya muda itakayotolewa.

Izingatiwe kwamba, pindi mstahiki wa msamaha aliyepatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018 atashindwa kutekeleza sehemu ya masharti ya mkataba wa makubaliano wa malipo, Kamishna Mkuu atabatilisha mkataba wa makubaliano wa malipo na kudai kiasi cha kodi kilichosalia kama vile hakukuwa na msamaha alioutoa. Aidha, hatua za ukusanyaji zitachukuliwa kuanzia tarehe 2/1/2020 bila taarifa nyingine.

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

**Dr. Edwin P. Mhede Ph.D**
**KAMISHNA MKUU**

215445702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars imulikwe safu ya ushambuliaji si Manula

**TAYARI** Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mrundi Etienne Ndayiragige, ameita kikosi chake kwa ajili ya mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Rwanda kujiandaa na mchezo wa marudiano dhidi ya Sudan kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Stars itarudiana na Sudan nchini humo Oktoba 18, mwaka huu ikihitaji ushindi zaidi ya bao 1-0 ili kuweza kufuzu fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Cameroon.

Hiyo ni kutokana na mechi ya awali Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kukubali kipigo cha bao 1-0 jambo ambalo linaifanya Stars kulazimika kupata matokeo zaidi ya hayo ili kuweza kufuzu fainali hizo kwa mara ya kwanza tangu 2009.

Hata hivyo, baada ya Ndayiragije kutangaza kikosi chake kitakachoingia kambini kujiwinda na mechi hiyo, kumezuka mjadala mkubwa kutoka kwa wachambuzi na wadau wa soka wakihoji sababu ya kutoitwa kwa kipa wa Simba, Aishi Manula na badala yake kuendelea kumwamini mlinda mlango mkongwe, Juma Kaseja wa KMC FC sambamba na Metacha Mnata wa Yanga.

Hakuna asiyeukubali uwezo wa Kaseja na zaidi kazi kubwa aliyoifanya hadi kuifikisha Stars katika hatua hiyo kufuatia kuiongoza kuitoa timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars. Katika mchezo huo timu hizo zilitoka sare tasa nyumbani na ugenini kabla Taifa Stars kuvuka kwa mikwaju ya penalti 4-1, huku Kaseja akiibuka shujaa kwa kudaka penalti mbili.

Lakini pia akafanya kazi kubwa tena dhidi ya Burundi kwenye mechi ya kuwania kufuzu kushiriki hatua ya makundi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

Katika mechi hiyo ambayo ugenini ilimalizika kwa sare ya bao 1-1 na mchezo wa marudiano Uwanja wa Taifa matokeo yakawa kama hayo, Kaseja aliibuka tena shujaa kwa kucheza penalti hatua ya matuta wakati wakivuka kwa penalti 3-0.

Lakini pia wote tumekuwa mashuhuda kwa uwezo unaoonyeshwa na Mnata katika kikosi cha Yanga hususan kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa ambayo kwa sasa wametolewa na kuangukia Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa mantiki hiyo, Nipashe hatuoni pengo lolote katika nafasi ya kipa kwenye kikosi hicho cha Ndayiragije na badala yake idara ambayo tunaona inahitaji kumulikwa zaidi ni ile ya ushambuliaji.


Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba katika mechi zote tano ambazo Ndayiragije ameiongoza Stars, mbili dhidi ya Harambee Stars na idadi kama hiyo dhidi ya Burundi pamoja na dhidi ya Sudan, tatizo kubwa limekuwa kwenye safu ya ushambuliaji kushindwa kucheka na nyavu. Takwimu haziongopi, dhidi ya Harambee Stars sare tasa nyumbani na ugenini, dhidi ya Burundi bao 1-1 ugenini na nyumbani kabla ya kulala bao 1-0 dhidi ya Sudan Uwanja wa Taifa.

Kulingana na takwimu hapo, ni wazi safu ya ulinzi ukianzia langoni kwa Kaseja, imekuwa imara zaidi na udhaifu mkubwa umekuwa kwenye ushambuliaji, idara ambayo kama si kumulikwa basi inahitaji mjadala wa kitaifa.

Katika mechi zote tano, washambuliaji wamekuwa wakishindwa kuzitumia nafasi wanazotengenezewa kutoka kwa viungo, jambo ambalo kwa sasa kwetu sisi kusikia wadau wa soka wakianza kuhoji nafasi ya Malula Stars tunaona halina mashiko kabisa.

Hatusemi Manula hana uwezo, bali makipa waliopo wana ubora wa kutosha, hivyo kwa sasa tusimvuruge Ndayiragije tumuache apambane kukisuka kikosi chake na kama ni maoni ya kukiboresha basi kwa mchezaji atakayeweza kuisaidia Stars katika safu ya ushambuliaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Umoja Yanga unahitajika sasa, si chokochoko za migogoro

Na Adam Fungamwango

**TIMU** inapotetereka kidogo, kuna baadhi ya wanachama ambao wanakuwa kwenye klabu kimaslahi na kuanzisha chokochoko zao.

Na tayari kuna baadhi ya wanachama wa klabu ya Yanga wamesikika wakianza chokochoko na kumtuhumu Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla kuwa anaipeleka klabu pabaya.

Hii ni baada ya timu hiyo kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, pamoja na kutopata ushindi kwenye mechi mbili za kwanza za Ligi Kuu, ikifungwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, na kupata sare ya mabao 3-3 dhidi ya Polisi Tanzania.

Kikubwa zaidi wanadai kuwa hivi sasa haelewani na Makamu wake, Fredrick Mwakalebela.

Wanachama hawa wamekuwa wakisambaza taarifa hizi kwenye mitandao ya kijamii, kiasi cha kuwachanganya na kuwavuruga baadhi ya wanachama wengine wa klabu hiyo.

Kwa bahati nzuri, Dk. Msolla mwenyewe amejibu kuwa wanaoeneza habari hizo ni baadhi ya wanachama wakaa milangoni ambao hawajalipwa pesa zao.

Akasema kuwa ni kweli baadhi ya wanachama hawajalipwa, lakini ni suala la muda kwani klabu ina mpangilio wake wa kufanya kazi na kulipa madeni.

"Haiwezekani uache kulipa mishahara ya wachezaji na benchi la ufundi ukawalipe wakaa milangoni. Siyo kama hatutowalipa, lakini kwanza inabidi wasubiri walipwe kwanza wachezaji halafu wengine watafuata," alisema mwenyekiti huyo.

Hapa inaonyesha kuwa ni suala la maslahi tu. Kuna baadhi ya wanachama hawajalipwa, sasa hasira zao wanapeleka kwa mwenyekiti.

**Wanachama hawa wamekuwa wakisambaza taarifa hizi kwenye mitandao ya kijamii, kiasi cha kuwachanganya na kuwavuruga baadhi ya wanachama wengine wa klabu hiyo. Kwa bahati nzuri, Dk. Msolla mwenyewe amejibu kuwa wanaoeneza habari hizo ni baadhi ya wanachama wakaa milangoni ambao hawajalipwa pesa zao.**

Hili ni tatizo ambalo lipo muda mrefu kwenye klabu hizi kubwa za Simba na Yanga. Kuna wanachama ambao kazi yao ni kutengeneza migogoro tu pale wanapoona maslahi yao yameguswa, yapo hatarini au yanacheleweshwa.

Kwa bahati njema tu ni kwamba kwa upande wa Simba suala hili linaweza kuwa ni historia kwa sasa kwani ilipobadilishwa katiba na kwenda kwenye mfumo wa uwekezaji, wanachama wa Simba wamekuwa hawana nguvu ya kikatiba kama ile ya zamani na sasa Yanga imebaki na katiba ile ile ya zamani ambayo mwanachama mmoja tu anaweza kulianzisha ikawa balaa.

Kwa siku za karibuni Yanga imepitia kwenye kipindi kigumu, lakini inaonekana kuna baadhi ya wanachama wanatumia kipindi hiki kutaka kutengeneza mgogoro, badala ya kuwa wamoja na kuangalia wapi walipokosea.

Hii inaonyesha kuwa wapo baadhi ya wanachama wa klabu hiyo wanapenda timu ifanye vibaya ili wapate fursa ya kuwasema na kuwachafua viongozi wao kwa sababu zao binafsi.

Simba ilitolewa mapema tu kwenye Ligi ya Mabingwa, pamoja na kwamba wanachama na mashabiki waliumia sana, lakini wameendelea kuwa wamoja kiasi kwamba wameanza vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kama kuna tatizo, kuna vikao ambavyo wanachama hukutana na viongozi wao na si kulumbana kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

# BARUA & MJADALA

## *Wakazi Kilimanjaro tuiache tabia hii*

**Mhariri**

*Habari za majukumu ya ujenzi wa Taifa,*

*NIMEJITOKEZA leo kwenye nafasi hii inayotupa fursa wananchi pamoja na mambo mengine ya kueleza kero na changamoto mbalimbali zinazotukabili kwenye maeneo yetu, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo mbele.*

*Kwa fursa hii, ninapenda kuzungumzia hatua isiyo ya kiungwana au kistaarabu inayofanywa na baadhi yetu sisi wazaliwa wa mkoa wa Kilimanjaro ambayo hata katika misahafu kwa wanaoamini haikubaliki.*

*Tayari watoto wetu, ambao ni wanafunzi waliokuwa wanasoma shule za misingi wamemaliza mitihani yao ya kitaifa katika ngazi hiyo ya elimu na kwa hali hiyo kwa sasa wako majumbani wakisubiri matokeo yao kwa ajili ya kujiunga na masomo ya sekondari.*

*Sasa wakati wa kipindi hiki wanachosubiri majibu, kuna utamaduni wa wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro na hasa sisi Wachaga ya kuchukua watoto hao ili waje watufanyie kazi zetu na hasa zile za kusimamia biashara mbalimbali kwa maana ya kuuza. Kimbembe huwa kinatokea wakati majibu ya mtihani huo yanapokuwa yametoka na kijana akawa amefaulu na kwa hali hiyo akahitajika sasa arudi nyumbani kwao tayari kwa ajili ya maandalizi ya kujiunga na kidato cha kwanza kwa masomo ya sekondari.*

*Mara nyingi 'matajiri wao' ama wenye biashara ambao wanakuwa wamewachukua watoto hao huwa wakati mwingine hawako tayari kuwaachia, wakitaka waendelee kuwauzia biashara zao.*

*Ndipo visa vya kwamba kuna mapungufu ya fedha kutoka kwenye biashara zao ama kuna mapungufu ya mitaji yaliyojitokeza baada ya kijana huyo kuwa ameanza kuisimamia biashara husika kabla hajaja.*

*Ndipo unakuta kijana wa watu anafanyiwa visa vya hapa na pale kwa lengo la kumkwamisha asiende kuendelea na masomo yake au hata kama anaondoka basi asiweze kulipwa haki yake ya mshahara aliyokuwa akiidai.*


*Ninatoa wito kwetu sisi wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro na hasa sisi Wachaga tumuogope Mungu, kwa maana tuachane na aina hii ya dhuluma ambayo baadhi ya wenzetu wamekuwa wakiifanya kwa muda mrefu sasa.*

*Ieleweke kuwa vijana hao huruhusiwa na wazazi ama walezi wao ili waje wajitafutie kipato cha kuwawezesha kujikimu katika kipindi wanachosubiri matokeo yao na tusitumie mwanya huo kuwadhulumu watoto hawa.*

**Deogratius Massawe - Rombo**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Timu za vijana safi, Stars tatizo, tunakwama hapa

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA haijawahi kuwa na tatizo la vipaji kwenye mchezo wa soka. Hata wachezaji wakubwa kutoka nje ya nchi wanakiri hilo. Aliyekuwa Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Emmanuel Amunike alikiri na kusema Tanzania huenda ikawa na vipaji zaidi kwenye soka kuliko hata nchini kwao Nigeria ambako ndiko kunakotoka wachezaji wengi wanaotamba kwenye soka barani Ulaya.

Ndiyo maana haikushangaza sana Jumamosi iliyopita timu ya vijana chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes kutwaa Ubingwa kwa timu za umri huo kwa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa U-20) nchini Uganda.

Baada ya kutoa vipigo vitakatifu, Jumamosi iliichapa timu ya Taifa ya Kenya U-20 kwa bao 1-0 kwenye mechi ya fainali.

Mwishoni mwa mwaka jana, timu ya Taifa ya vijana chini ya miaka 17, Serengeti Boys ilitwaa Kombe la Cosafa nchini Afrika Kusini, huku pia ikiwa ndiyo bingwa wa Cecafa kwa umri huo.

Kwa muda mrefu Tanzani inatawala soka la Afrika Mashariki na Kati kwa vijana kuanzia chini ya miaka 17 mpaka 20.

Hata hivyo, mashabiki wengi wa Tanzania wamekuwa wakijiuliza ni kwa nini tunashindwa kufanya vizuri kimataifa hasa kwenye timu ya wakubwa, Taifa Stars?

Wanajiuliza kwa nini wachezaji hawa wasiwe ndiyo wachezaji wa Taifa Stars baada ya miaka michache ijayo?

Kwenye meza za magazeti na kwenye mitandao ya kijamii, wengi pamoja kuwapongeza vijana wetu, lakini wana wasiwasi kuwa baada ya muda fulani wachezaji hawa hawatoonekana tena na huenda watakaoonekana kucheza soka ni wachache.

Wanarudisha kumbukumbu nyuma, baadhi kwa wachezaji wa timu za vijana waliofanya vizuri, leo hii ni wachache sana wanaonekana wakiendelea kucheza soka la ushindani na anayeonekana sana ni Ramadhani Kabwili ambaye yuko Yanga.

Hapa linaonekana tatizo kuwa wachezaji wetu vijana wanashindwa kutoka kwenye ujana wakiwa na viwango vyao hadi kufika kwenye timu ya Taifa, Taifa Stars wakiwa kwenye viwango hivyo hivyo. Tatizo ni nini?

Kuna baadhi walishauri kuwa wachezaji hawa wasiachiwe kujiunga na timu za Ligi Kuu hasa Simba na Yanga kwa sababu zinaua vipaji. Na badala yake eti watunzwe na serikali na Shirikisho la Soka nchini (TFF). Hii si kweli. Serikali au TFF haiwezi kuwatunza au kuihudumia timu ambayo haiko kwenye michuano yoyote, eti tu kwa sababu isisambaratike. Ni gharama kubwa sana kufanya hivyo, tena isiyo ya lazima. Na pia huwezi kumzuia mchezaji kujiunga na klabu fulani kwa sababu hayo ni maisha yake binafsi.

Tatizo ninaloliona mimi ni mtambuka, si la serikali peke yake wala TFF, hapa mpaka wachezaji wenyewe na wazazi wanahusika kwa wachezaji vijana kupotelea kusikojulikana au viwango vya kushuka wanapokuwa kwenye umri wa kuichezea timu ya wakubwa.

Wachezaji wenyewe vijana wana tabia ya kulewa sifa na badala ya kujitunza wanajiachia, wakiwa na umri mdogo, hivyo kutoweza kufikia malengo.

Kingine ni baadhi ya wazazi kuwahimiza zaidi kwenye masomo wanayoyataka wao wasomee na kuwakataza kuendelea na mchezo wa soka, ambao wanaona ni kama unawapotezea muda wa masomo.

Maisha ya nyumbani ya watoto wengi ni ya chini, hivyo baadhi ya wachezaji kuanza kujitegemea kufanya kazi ambazo zitakazowaingizia pesa za haraka, kuliko soka ambalo itabidi asubiri miaka kadhaa ijayo huku akiwa hajui hatima yake.

Serikali kupitia wizara husika ya michezo pamoja na TFF wanapaswa sasa kuangalia uwezekano wa kutafuta nchi marafiki na washirika ili wawaombe wawatafutie 'academy' za kisasa ambazo zitaweza kuwachukua vijana hao na kuwatunza wakiendelea kusoma na kucheza soka, ili kuondokana na kuwapo kwenye mazingira ambayo yanaweza kusababisha kuachana na soka kwa sababu yoyote ile kama ilivyokuwa zamani nchi rafiki ya Cuba ilivyoisaidia Tanzania kuzalisha mabondia wengi na waliokuwa kwenye viwango vya juu Afrika na dunia.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Wanunuzi tanzanite waibua malalamiko

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

WANUNUZI wa kati na wadogo wa tanzanite wamedai madini hayo yameshuka bei kwa asilimia 50, kutokana na kupungua kwa wanunuzi wakubwa kutoka nje.

Adha, walidai kuwa `karate' moja ya tanzanite sasa inauzwa chini ya Sh. 300,000 wakati miaka ya nyuma iliuzwa kati ya Sh. 400,000 na Sh. 700,000.

Mwenyekiti wa umoja wa wanunuzi wa kati na wadogo Tanzania Bara (Tasigedo), Hamisi Lyoba, ndiye aliyetoa maelezo hayo katika mahojiano na Nipashe. Lyoba alisema kwa mtazamo wake mauzo yameshuka kati ya asilimia 45 hadi 50.

Aidha, aliongeza kuwa kushuka kwa bei hizo ni kazi ya ufuatiliaji mkubwa unaofanywa na serikali katika sekta ya madini tofauti na zamani.

"Hili linasababisha wanunuzi wa Thailand, Marekani, Ujerumani na Sirilanka kushindwa kuja nchini," alisema.

Lyoba, alitoa sababu nyingine kuwa ni mazoea ya kusafirisha tanzanite ghafi iliyokuwa inapelekwa nje ii kuzalisha ajira kwenye mataifa ya wanunuzi ili yakaongezewe thamani.

"Sababu nyingine ni kutofanyika maonyesho ya madini ya kimataifa kwa miaka mitatu mfululizo, ambayo yalikuwa yakileta wanunuzi wakubwa nacho ni kikwazo," alisema Lyioba.

Sababu nyingine ni kodi sumbufu, mathalani ya ongezeko la thamani (VAT) ambayo ni asilimia 18 na asilimia tano ya zuio la thamani ya mzigo kuendelea kutozwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini ((Tamida) Sammy Mollel, alipinga tanzanite kushuka bei.

Alisema kilichotokea ni kuongezeka uzalishaji hali inayosababisha madini hayo kujaa sokoni. "Madini ni mengi na yanaingia sokoni kwa wakati mmoja, hivyo wanunuzi wanapanga bei wanayoitaka," alisema Mollel. Akizungumzia maonyesho ya madini kutofanyika, alikiri kuwa kwa miaka miwili ya 2018 na 2019 alikiri kuwa hayajaandaliwa kutokana na mchakato wa mabadiliko ya sheria ya madini na kanuni zake.

Akifafanua kuhusu VAT na kodi ya zuio thamani ya mzigo kwa mkoa wa Arusha, alisema limekuwa kero kwa sababu viongozi hawakufuatilia.

"Kilichotokea hapa ni watendaji hawakufahamu kuwa ni sheria walisubiri waletewe waraka, wakati mikoa mingine kama Manyara walitekeleza bila kusubiri waraka. Ila tumelimaliza tulipozungumza nao," alisema Molleli.

Katibu wa chama cha wauzaji na wanunuzi wakubwa wa madini (Tamida), Benny Mtalemwa, aliomba serikali kuanzisha benki ya madini kusaidia kudhibiti bei za madini.

Alisema iwapo serikali itaanzisha benki hiyo, itawezesha wafanyabiashara wa tanzanite na madini mengine kuyahifadhi kwenye benki hiyo ili wayauze yakiwa na bei nzuri.

Alishauri benki hiyo ianzishwe na mifuko ya kijamii kama vile NSSF, PPF, LAPF, PSPF na wabia wengine.

Alisema itachocheo masoko makubwa ya bidhaa za madini yapatikane nchini na kurahisisha uuzaji na pia itatoa mikopo ya fedha, mashine za kisasa za uchimbaji na mitaji ya kufanya biashara kwa dhamana nafuu.

Pia alisema, benki hiyo itahifadhi madini kipindi cha anguko na hasara hadi wakati wa unafuu wa bei.

"Benki itaunganisha benki za nje na za ndani kwenye malipo na kusafirisha nyaraka za malipo, pia ni usalama wa fedha na madini, hasa kwa wazawa wanapotaka kufanya biashara nje ya nchi."

Kaimu Ofisa Madini Mfawidhi Mkoa wa Arusha, iliyo chini ya Wizara ya Mdini, Erick Robert, alisema hana uhakika na madai ya anguko la bei.

Aidha, alisema anaamini kuwa thamani ya madini imepanda kwa asilimia kubwa sasa baada ya serikali kujenga ukuta kudhibiti utoroshaji na madini na ukwepaji kodi na tozo nyingine.

**Imeandaliwa na Cynthia Mwilolezi, Sabuni Daniel na Zanura Mollel.**



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akiwa na Mbunge wa Mbulu, Flatei Massay (kulia), wakipewa maelezo kutoka kwa Eliminata Awet kuhusu nyumba za Wadatooga, walipotembelea kujionea nyumba ya kabila hilo katika kituo cha utamaduni cha Haydom kabla ya kufunga maonyesho yaliyoshirikisha ngoma za makabila 30 ya kutoka mikoa mbalimbali nchini. **MPIGAPICHA WETU**

# Wapewa mbinu kuepuka mafataki

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WANAFUNZI wa kike wa Shule ya Sekondari Qash iliyopo Halmashauri ya Babati mkoani Manyara wamepewa mbinu za kukwepa mafataki wanaowarubuni na kuwafanya wakatishe ndoto zao.

Mbinu hizo zikitolewa na Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) na Mjumbe wa kamati ya elimu, afya, malezi na mafunzo, Magreth Maina wakati akizungumza na wasichana wa shule hiyo wakati alipowatembelea.

Maina aliwashauri kuepuka tamaa na vishawishi wanavyopatiwa na mafataki, ili watimize ndoto zao za kuwa wabunge, madaktari, walimu na wakurugenzi.

"Ukikutana na kijana au mwanaume akakulubuni kwa fedha ukakubali mwishowe atakuingiza mkenge mtafanya ngono na utabeba mimba na shule ndio mwisho wake hivyo wakatalieni," alisema Maina na kuongeza:

"Ukitaka kuwa na nafasi nzuri ya cheo ni lazima uwe mvumilivu, hivyo vumilieni msibebe mimba za utotoni maana zitaharibu malengo yako."

Aidha, aliwataka kujiamini katika masomo yao na kutokubali pale wanapokutana na wanaowarubuni.

Maina alipokuwa akitoa elimu hiyo shuleni hapo aliambatana na wajumbe wa kamati ya utekelezaji ya Wilaya ya Babati ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Umoja wa Wanawake Tanzania na wakatumia fursa hiyo kugawa pedi kwa wanafunzi hao.

Naye Mwalimu Mlezi, Hosana Kitumu, alisema tokea Januari hadi Oktoba mwaka huu wanafunzi waliobeba mimba ni wanafunzi wanne.

# Serikali yashtukia upotevu wa ngozi ghafi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imesema ngozi ghafi inayotokana na mazao ya mifugo, zaidi ya vipande milioni nane havijulikani vinakwenda wapi, kati ya vipande milioni 10 vinavyozalishwa nchini.

Kutokana na hali hiyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanza kutoa ilani yake kwamba kila mchunaji wa ngozi nchini ni lazima asajiliwe na kupata leseni, kwa vile muda mfupi ujao haitaruhusu mtu ambaye hana leseni kumshika mnyama wala kumchuna kama hajafuata taratibu za kisheria. Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo, Usalama wa Chakula na Lishe wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Gabriel Bura, alisema ngozi ambazo zinaingia katika mfumo rasmi wa biashara na serikali inapata kodi katika hivyo vipande hivyo milioni 10 vinavyozalishwa ni vipande milioni 1.5

Bura alikuwa akizungumza kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki na wachunaji wa ngozi, wafanyabiashara ya mazao ya mifugo na wenye viwanda vya ngozi katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

"Vipande hivyo, ndivyo ambavyo vinaingia Mamlaka ya Mapato (TRA) na kuruhusiwa kusafirishwa kama ngozi ghafi iliyosindikwa, vingine vyote milioni nane havijulikani vinakwenda wapi? Labda vinatoroshwa kwenda nje kupitia kwenye mipaka au vingine vinatupwa kwa kukosa soko, nyingine zinaharibiwa vile vile kutoka kwenye machinjio.

Zaidi Bura alieleza: "Tumekuja kuwaambia kwamba mnatambuliwa kisheria na tumekuja kuweleza sheria inasema nini kuhusu nyie, ili sasa mtu mwingine asiruhusiwe kumshika mnyama wala kumchuna kama hajafuata zile taratibu za kisheria."

Katika taarifa yake, mkurugenzi huyo ameeleza kuwa Tanzania inazalisha ngozi za ng'ombe milioni nne kwa mwaka, ng'ozi za mbuzi milioni 5.6 na ngozi za kondoo milioni moja.

Akiwa katika Mkoa wa Kilimanjaro, Mkurugenzi huyo alisema takwimu zinaonyesha kati ya asilimia 40 mpaka 60 za uharibifu wa ngozi unatokea kwenye machinjio kutokana na ngozi kuoza kutokana na uharibifu wa ngozi kukatwa vibaya au kutobolewa.

Aidha, takwimu za idara hiyo zinanyesha kuwa Tanzania ina mifugo mingi ikiwamo ng'ombe milioni 32, mbuzi milioni 20, kondoo milioni tano na kuku milioni 80. Akijenga hoja kuhusu umuhimu wa kusajiiwa na kupata eseni hizo kwa wachunaji wa ngozi, Mkurugenzi huyo alisema Tanzania ina uwezo wa kuzalisha vipande vya pea (jozi) za viatu na mikanda milioni 1.7

Kutokana na hai hiyo, Bura ameeleza kuwa wakati huo huo, taifa inaagiza pea za viatu milioni 40 kwa mwaka na hivyo kutumia fedha nyingi sana kwenye kuagiza viatu, wakati sisi tunazalisha vipande vya ngozi milioni 1.7.

HABARI KITAIFA

# Wanawake CUF wahamasishwa kugombea 2020

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimewataka kinamama kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu 2020, ili kutetea haki zao katika vyombo vya kutunga sheria.

Hayo yalielezwa na Mdhamini wa Bodi ya CUF, Asha Said, alipokuwa akizungumza na wanachama wa Jimbo la Chonga kwenye ufunguzi wa tawi jipya katika Shehia ya Chonga Wilaya ya Chakechake.

Alieleza kuwa bado wanawake wamekuwa nyuma katika kugombea nafasi mbalimbali ndani ya chama, lakini pia hata katika uchaguzi mkuu.

"Tusikubali kuwaachia kinababa peke yao kuchukua fomu za uongozi katika uchaguzi ujao, na sisi tusimame kidete katika kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ili tuweze kuwasidia kinamama wenzetu," alisema Asha.

Aidha, CUF imewaomba kinamama ambao wanapata fursa ya kuchaguliwa na kuingia katika vyombo vya kutunga sheria kuwa imara na kuwaletea kinamama wenzao.

Aliwataka wanawake hao kujikusanya pamoja katika kuanzisha vikundi vya ushirika ambavyo vitaweza kuwaletea maendeleo na kuwainua kimaisha. "Lakini pia niwaombe na vijana wenzangu tusikubali kukaa maskani bure bila ya kazi muhimu na sisi tukae pamoja na tubuni mbinu ambazo zitaweza kutusaidia katika harakati zetu za maisha na chama chenu kitawaunga mkono," alisema Asha.

Naye Naibu Mkurugenzi Mipango na Uchaguzi Taifa, Mohammed Vuai Makame, aliwahakikishia wanachama hao kuwa CUF bado ipo na inafanya kazi zake kama kawaida licha ya maneno yanayodaiwa na baadhi ya watu kuwa chama hicho kimekufa.

Alisema kuwa juhudi kubwa ambazo CUF inataka kufanya ni kuwasaidia wanachama wake ambao watajikusanya pamoja na kuanzisha miradi ya maendeleo hasa katika mambo ya kilimo na uvuvi kwa kuwapatia nyenzo za kujiendeshea.

"CUF ni chama kikongwe na kimepitia misukosuko mingi, ila bado kipo na kitaendelea kuwapo, cha msingi niwaombe wanachama wenzangu tusirudi nyuma wala tusikate tamaa," alisema Vuai.

Naye Naibu Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa chama hicho, Mbarouk Seif Salim, akiwataka wanachama hao kuwaelimisha wananchi wengine ambao wamekihama chama hicho kurudi ili waweze kukijenga upya.



Meneja Masoko na Mawasiliano wa GSM Group, Matina Nkurlu (aliyevaa koti), akisalimiana na Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kaole ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani, Athumani Idd, baada ya shule yao kukabidhiwa msaada wa mabati kwa ajili ya kuezekea madarasa ambayo yanavuja kiasi cha kuwafanya wanafunzi kusoma kwa shida. Kushoto ni Mlezi wa Shule, Fimbo Butale. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilimo korosho Singida chamgusa Waziri Mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekagua shamba la mfano la korosho lenye ukubwa ekari 12,000 lililopo kijiji cha Misigati, wilayani Manyoni na kusema kuwa ameridhishwa na uamuzi wa wilaya hiyo kuwa na zao mbadala la biashara.

Akizungumza na wananchi na baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo waliokuwapo eneo hilo mwishoni mwa wiki, Waziri Mkuu alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, kwa kulibeba wazo hilo na kuhakikisha linatimia.

"Nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa kulibeba jambo hili, lakini nikuombe wewe na viongozi wenzako mhamasishe wengine walime zaidi zao hili kwa sababu korosho ni zao kubwa duniani na tena zao hili lina bei nzuri kimataifa," alisema.

Alisema anatambua kwamba timu ya wataalamu kutoka kituo cha utafiti wa kilimo cha Naliendele, Mtwara imeshawasili Manyoni ili kufanya utafiti wa zao hilo na jinsi linavyoweza kuzaa mara mbili kwa mwaka.

"Kwa kawaida, mkorosho mmoja hutoa kilo 40 za korosho kwa msimu mmoja, kwa hiyo kwa msimu miwili mtapata kilo 80. Ninawasihi limeni korosho kwa ajili ya watoto wenu ambao wako darasa la pili au la tatu.

Mkulima ukianza kuvuna, utaendelea kuvuna kwa miaka 20 mfululizo na kwa hiyo hao watoto hawatahitaji kulipiwa ada wakiwa chuo kikuu sababu korosho itakuwa inawalipia," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amewataka wakulima wanaolima zao hilo wilayani Manyoni, waunde ushirika wao ambao utawasaidia kuagiza dawa kwa pamoja ama kuuza kwa pamoja kwa pamoja.

Hivyo, amemwagiza Ofisa Ushirika wa Wilaya hiyo, Yusta Philipo, ahakikishe anasimamia jambo hilo kuanzia sasa.

Mapema, akitoa taarifa juu ya mradi huo, Meneja wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) Kanda ya Kati, Ray Mtangi, alimweleza Waziri Mkuu kwamba mradi wa kilimo cha korosho unajumuisha mashamba makubwa mawili ambapo shamba la Misigati lina ukubwa wa ekari 7,000 na lile la Mikwese lenye ukubwa wa ekari 5,000.

# Mkakati wa kumn'goa Mch. Msigwa

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeanza mikakati ya kurejesha Jimbo la Iringa Mjini linaloshikiliwa na Mchungaji Peter Msigwa kupitia Chadema, kwa kutoa mafunzo maalum kwa wanachama wake.

Kulekea uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na uchaguzi mkuu wa 2020 wana-CCM wamekumbushwa kujenga umoja na mshikamano, jambo ambalo ni la msingi katika kushinda chaguzi zote.

Hayo yalisemwa na Naibu Katibu Mkuu CCM Bara, Rodrick Mpogolo, wakati wa mkutano wa ndani wa CCM Wilaya ya Iringa Mjini kwa ajili ya kuzindua mkakati maalum wa mabalozi mkakatini.

Alisema kazi ya kwanza ya msingi ni mwanachama wa CCM kujenga umoja na mshikamano pamoja na mwanachama kupigia kura chama chake, na kuongeza kuwa anayepigia kura upinzani ni msaliti.

Mpogolo pia aliwataka mabalozi kuwa na wanachama 100 kwa sababu uchaguzi maana yake ni namba.

Aliongeza kuwa ili kupata ushindi katika mitaa yote ndani ya Manispaa ya Iringa, wanahitaji kura nyingi ambazo kila balozi akiwa na wanachama 100 kwa mashina 482, maana yake kuna jumla ya kura 48,200.

"Balozi wa CCM aheshimiwe maana yeye ndiyo bosi na apewe heshima zote maana ndiyo msingi wa chama chetu," asisitiza Mpogolo.

Aliwataka mabalozi wote Mkoa wa Iringa kuhakikisha kila mmoja anakuwa na wanachama wasiopungua 100 ikiwa ni msingi wa chama na mbinu za kulinda uhai wa chama.

Aidha, alisema kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu CCM itashinda mitaa yote, vijiji vyote na vitongoji vyote kwa kuwa wananchi wametambua kazi kubwa iliyofanywa na serikali.

Mwenyekiti ya CCM Iringa Mjini, Said Rubbeya, alisema mkakati huo umezinduliwa jimboni humo kwa chama hicho kutoa mafunzo mbalimabli kwa mabalozi wa nyumba 10 kuhusu msingi wa chama na mbinu za kulinda uhai wa chama.

# Mkoa wataka vifaa vya uchaguzi kabla ya mvua

**Na Tiganya Vincent,**
TABORA

KAMATI ya Usalama mkoani Tabora imezitaka halmashauri zote kuhakikisha zinapeleka mapema vifaa kwa ajili ya upigaji wa kura za uchaguzi wa serikali za mitaa kabla ya mvua haijaanza kunyesha ili kuwawezesha wananchi wenye sifa kushiriki.

Maelekezo hayo yalitolewa jana wilayani Igunga na Mkuu wa Mkoa huo, Aggrey Mwanri, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilipokuwa katika ukaguzi wa maeneo ya kujiandikishia na vifaa vya kupigia kura.

Alisema kuna maeneo mengine kwenye wilaya mbalimbali hasa za Igunga ni vigumu kufikika kwa magari labda kwa miguu katika kipindi cha masika.

"Hakikisheni masanduku na vifaa vingine vinavyotakiwa vinafika katika vituo vya kupigia kura mapema...mkizembea na mvua zikiaanza kunyesha njia hazitakuwa zikipitika kwa magari... jambo linaloweza kusababisha baadhi ya wananchi kushindwa kupiga kura," alisema.

Naye Katibu wa Kamati hiyo, Msalika Makungu, aliwaagiza maofisa uchaguzi kuhakikisha wanabandika matangazo katika maeneo mengi yanayohamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha na wakati wa upigaji kura. Alisema hakuna sababu ya kuwa na matangazo katika maeneo machache wakati serikali imetoa fedha kwa ajili ya shughuli hizo. Makungu alisema serikali itafuatilia ili kuona kama fedha zilizotolewa kwa ajili ya matangazo na uhamasishaji wananchi zimetumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kama itabainika kwenye kinyume cha makusudi haitasita kuchukua hatua.

Wakati huo huo, Kamati ya Usalama imesema ni marufuku mtu asiye raia wa Tanzania kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mwanri alisema ni jukumu la wananchi kuwafichua watu ambao sio Watanzania watakuwa wakitaka kujiandikisha au kuchukua fomu ili hatua kali dhidi yao ziweze kuchukuliwa.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu (katikati), akizungumza na mmoja wa wateja wa benki hiyo, kupitia simu alipotembelea chumba cha mawasiliano kwa wateja (Call Centre) cha benki hiyo wakati wa maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Amana wa benki hiyo, Agnes Kaganda (kushoto). **MPIGAPICHA WETU**

# Fursa ajira kwa wanaosoma sayansi

**Na Suleiman Rashid Omar,**
PEMBA

WANANCHI wa Zanzibar wametakiwa kushirikiana na Taasisi ya Milele Foundation kuwandaa na kuwahamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi ili kukabiliana na ushindani wa soko la ajira la Afrika Mashariki.

Haya yameelezwa na meneja wa mradi wa kuhamasisha wanafunzi wa kike, kupenda kusoma masomo ya sayansi (stem), Ali Mohamed Abdallah, kwenye mkutano wa wadau wa mafanikio ya stem wakiwamo wanafunzi, walimu, asasi zizizo za kiserikali na taasisi za serikali mjini Chakechake.

"Jamani kama hatukujiandaa tukabaki kama tulivyo, minakwambieni tunaweza kuachwa nyuma na ajira zote muhimu kuchukuliwa na wageni na kuishia kulalamika," alisema Ali Mohamed. Alisema mradi huo umelenga kuwapa mbinu walimu za ufundishaji wanafunzi kuwahamasisha kuyapenda masomo ya sayansi ambayo ni muhimu katika kuingia kwenye soko la ajira.

Alisema Tanzania imeingia katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), hivyo Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Tanzania ni wakati mwafaka wa kuendelea kuwatayarisha vijana wa Kizanzibari, kukabiliana na changamoto za ajira katika nyanja mbali mbali za kiuchumi.

Mkutano huo ulio shirikisha wafanyakazi wa tasisi zinazohitaji watu waliohitimu masomo ya sayansi ili kuwaelezea jinsi wanavyofanya kazi zao na iwapo kuna nafasi ambazo wahitimu wa masomo ya sayansi wanaweza kuzipata kama moja ya njia ya kuwahamasisha wanafunzi hao.

Suleiman Makame kutoka Maabara ya Jamii Wawi, aliwaelezea wanafunzi hao kuwa maabara yao ina nafasi nyingi kwa wanafunzi watakaohitimu masomo ya sayansi.

Aliwataka kuongeza bidii katika masomo hayo ili kuona wanashika nafasi hizo zenye lengo la kumkomboa kijana na changamoto za ajira.

Fundi Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Khamis Ali, aliwataka wanafunzi hao kusoma masomo ya sayansi kwani idara zao zinahitaji wanafunzi waliosoma sayansi.

Juma Musa Juma, mwakilishi wa Shiriki wa Utangazaji Zanzibar (ZBC) alisema wanafunzi wa sayansi wanahitajika sana katika shirika lao.

Mkuu wa Miradi ya Milele Zanzibar Foundation, Khadija Ahmed Sharif, alisema hatua ya kuwahamasisha vijana kusoma masomo ya sayansi inawahusu wananchi wote, kwani hiyo ndio fursa pekee ya kuwajengea mustakabali bora wa kimaendeleo.

# Sagcot yawapa 5 wabia ujenzi wa miundombinu

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini (Sagcot), kimepongeza hatua mbali mbali zinazochukuliwa na wabia wake katika ujenzi wa miundombinu kwenye kongani za kituo hicho.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga, kongani hizo Ihemi, Mbarali na Kilombero.

Akizungumza mjini Dar es Salaam, Kirenga alisema kuwapo kwa miundombinu kunachochea uzalishaji na kuimarisha masoko ya mazao, hivyo kukifanya kilimo kiwe chenye tija.

"Tunawashukuru wabia wetu ambao tumekuwa tukishirikiana nao katika kufanya kazi ya kuhakikisha mkulima anakuwa na usalama wa chakula na kujipatia kipato cha kutosha, hayo yanachagizwa na kuzidi kuimarika kwa miundombinu iliyojengwa na serikali, sekta binafsi na wadau wetu wa maendeleo,'' alisema.

Alisema kuimarika kwa miundombinu na urahisi wa kupata masoko ya mazao ambalo ni jambo muhimu katika kutekeleza azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

"Hali ni nzuri katika mikoa ya Iringa, Mbeya na katika maeneo ya kongani zingine. Tunaamini uwepo wa miundombinu na uhakika wa masoko itachochea sana katika kutekeleza azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alisema Kirenga.

Alisema uboreshwaji wa miundombinu katika maeneo ya uzalishaji yatachochea zaidi uanzishwaji wa viwanda na kupelekea maendeleo katika maeneo ya vijijini kwa kutoa nafasi za ajira na uhakika wa soko la mazao ya wakulima.

"Tija katika uzalishaji wa mazao itazidi kuongezeka kutokana na miundombinu mbalimbali kuboreshwa na ushiriki wa wadau mabalimbali wa maendeleo katika kukuza na kuendeleza sekta ya kilimo ambayo ni kichocheo cha ujenzi wa viwanda," alisema.

Aidha, Kirenga ameipongeza serikali kwa kuimarisha Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA), na kueleza kwamba kupatikana kwa umeme vijijini kumechochea ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao na kuongeza thamani ya mazao hayo.

Ameishukuru kipekee Taasisi ya Utafiti Tanzania (TARI) kwa tafiti za mbegu ili kuongeza ubora na tija katika kilimo cha kisasa.

# Bil. 400/- kuwapa maji wananchi 800,000

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

ZAIDI ya wananchi 800,000 wa Mkoa wa Simiyu, wanatarajia kunufaika na mradi wa maji ambao utajengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 400.

Fedha hizo zitachangiwa na wadau wa maendeleo ikiwamo Ujerumani, Serikali ya Tanzania na nguvu kazi ya wananchi.

Hayo yalielezwa jijini Mwanza na Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, baada ya kupokea ujumbe wa Kamati ya Mazingira na Udhibiti wa Viumbe wa Bunge la Ujerumani lililoongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Syevia Kothing-uhl, ambao wamefanya ziara mkoani Simiyu.

Lengo lilikuwa kutembelea maeneo yatakayojengwa mradi wa maji wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi ambao pia walipata fursa ya kutembelea miradi ya mfumo wa utoaji majitaka maeneo ya miinuko na mabwawa ya kutibu majitaka mkoani Mwanza.

Aweso alisema lengo kuu la mradi huo ni kuboresha afya na kuongeza uzalishaji mali ili kuinua hali ya maisha ya wananchi walioathirika na mabadiliko ya tabia katika maeneo husika ya mradi.

"Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa maeneo ambayo yanakabiliwa na changamoto ya maji, hivyo ufadhili huu wa zaidi ya Sh. bilioni 400 uliotolewa na Benki ya Ujerumani (KFW), mfuko wa mabadiliko ya tabianchi ya Ujerumani na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji mkoani humo utakuwa mkombozi kwa wananchi wa mkoani humo," alisema.

"Licha ya kupata maji ambayo watatumia katika shughuli mbalimbali pia mradi utasaidia katika kilimo cha umwagiliaji ambapo zaidi ya wananchi 800,000 pamoja na vijiji 200 ambavyo vitapitiwa na bomba kuu vitanufaika, hivyo serikali imedhamiria kumtua ndoo mama kichwani katika mradi huu, itaendelea kuchangia fedha zenye thamani ya Euro milioni 40 kwa ajili ya kuhakikisha mradi unafanikiwa," alisema Aweso.

Alisema ameagiza wataalamu waanze mchakato haraka ili ujenzi uanze kutekelezwa kwani fedha zipo na wananchi wa maeneo hayo waweze kunufaika, huku wakiendelea kufanya shughuli zao za kilimo ambazo zitawasaidia katika kuinua uchumi na hali zao za maisha.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, alisema, mradi huo utatekelezwa katika wilaya zote tano za mkoa huo ambao utatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itahusu wilaya za Busega, Bariadi na Itilima, huku ya pili itahusu wilaya zote zitakazokuwa zimebaki ambazo ni Meatu na Maswa.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji wa Bunge, Mahmoud Mgimwa, alisema Mei 3, mwaka huu walisaini mkataba wa Sh. bilioni 444 wa mradi wa maji mkoani Simiyu ambao ni miongoni mwa miradi mikubwa nchini.



Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye (katikati), akiielekeza kampuni ya Vodacom kuhamisha mnara na ujengwe eneo la shule ili kuepusha mgogoro na mmiliki wa eneo ulipojengwa mnara huo, wakati wa ziara yake kwenye mnara huo, kijiji cha Bukuku, Kata ya Rufita wilayani Nyang'hwale, Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 2/- kila kijiji ujenzi wa hospitali ya wilaya

**Na Sabato Kasika**

WAKAZI wa Jimbo la Musoma Vijijini, mkoani Mara, wameunga mkono juhudi za serikali kwa kuchangia Sh. milioni mbili kila kijiji kwa ajili ya kuharakisha ujenzi wa hospitali ya wilaya yao.

Kiasi hicho ni michango ya fedha taslimu au kutoka katika asilimia 20 ya fedha zinazorejeshwa na halmashauri yao kutoka kwenye makusanyo ya mapato yao ya ndani.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Musoma, Charles Magoma, aliliambia gazeti hili kuwa serikali kuu ilishatoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo.

Akifafanua zaidi kuhusu michango hiyo, Magoma alisema, Jimbo la Musoma Vijijini lina vijiji 68 na kwamba 33 kati ya hivyo, vina vyanzo vya mapato na vimekubali asilimia 20 inayorejeshwa na halmashauri katika kila kijiji kwa ajili ya maendeleo ibaki huko kama mchango wa ujenzi wa hospitali. "Vijiji ambavyo havina vyanzo vya mapato ni 35, na kila kijiji kinachangia kila kimoja Sh. milioni mbili na hivyo jumla ya fedha zote tunazotarajia kupata kutoka vijiji vyote 68 ni Sh. milioni 136," alisema Magoma.

Magoma alisema, hospitali hiyo inajengwa kwenye kitongoji cha Kwikonero, katika kijiji cha Suguti, Kata ya Suguti na huku baadhi ya majengo yakiwa tayari yameezekwa.

"Wakati wananchi wakichangia kiasi hicho cha fedha, mbunge wao Profesa Sospeter Muhongo ameanza kuchangia kwa kutoa saruji mifuko 100 na ataitoa muda wowote itakapohitajika," alisema Magoma.

Aidha, mwenyekiti huyo alisema, wananchi wanaishukuru serikali kuu kwa kutoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo, ambayo itakuwa ni mkombozi kwao kwa matatizo ya kiafya.

"Wananchi hao pia wanawashukuru Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vicent Anney na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, John Kayombo kwa uongozi wao kwa jinsi wanavyosimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo Musoma Vijijini," alisema.

Alisema, chini ya uongozi wao, kwa sasa Musoma Vijijini kuna vituo viwili vya afya, vya Murangi na Mugango, huku zahanati za serikali zinatoa huduma zikiwa ni 24, za binafsi nne na zinazojengwa ni 13.

"Nguvukazi ya wananchi, serikali, mbunge na wadau wengine wa maendeleo imesaidia kulifanya jimbo kupiga hatua, na sasa kuna kituo cha afya kinajengwa katika kijiji cha Nyambono," alisema.

Magoma alisema, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020 inatekelezwa kwa kasi kubwa ili kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati moja.

# Elimu juu kupata mikopo bila riba

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wa vyuo vikuu vya ndani wametangaziwa fursa, baada ya kampuni moja kueleza kuwa itaanza kuwapa mikopo bila riba.

Lengo la mikopo bila riba ni kuwapa unafuu wazazi wanaoshindwa kusomesha watoto wao.

Fursa hiyo ilitangazwa na Kampuni ya Global Education Link, ambayo inatoa mikopo hiyo kwa wanafunzi inaowaunganisha kwenda kusoma vyuo vikuu vya nje ya nchi na wazazi wao hurejesha kwa awamu tofauti bila kutozwa riba.

Ahadi hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Abdulmalik Mollel, jijini Dar es Salaam katika mahafali ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari Tusiime.

Mollel alisema kampuni yake imefikiria kuanza kutoa mikopo hiyo baada ya kuwepo kwa mahitaji hayo kwa baadhi ya wazazi wanaotaka kusomesha watoto wao kushindwa kufanya hivyo kwa kukosa ada.

"Nimesikia changamoto ya ada kwenye risala ya mwalimu mkuu wa Tusiime kwa hiyo Global Education Link inajipanga kuangalia uwezekano wa kuanza kutoa mikopo isiyo na riba kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya ndani," alisema.

Mollel alisema serikali imekuwa ikifanya kazi kubwa kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo elimu, hivyo ni muhimu kwa wadau kuendelea kumuunga mkono kufanikisha malengo yake.

"Mheshimiwa Rais Magufuli anasifika dunia nzima kwa kazi kubwa anayoifanya hapa nchini na watu wengi wamekuwa wakija Tanzania kujifunza mambo mbalimbali hii yote ni kutokana na uwezo mkubwa wa utendaji wa Rais wetu John Magufuli," alisema.

Mollel aliahidi kutoa mifuko 400 ya saruji kusaidia ujenzi wa bwalo katika shule hiyo na kununua vitabu 1,000 vya mwanafunzi wa shule hiyo na kuviweka kwenye maktaba ya shule hiyo.

## Waziri atoa neno kambi kitaaluma

**Na Happy Severine,** BARIADI

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mary Mwanjelwa, ametoa wito kwa wanafunzi wa kidato cha nne mkoani Simiyu ambao walipata ufaulu hafifu katika mtihani wa utimilifu (mock) walioko kambi ya kitaaluma kutumia fursa hiyo kusoma kwa bidii ili waweze kutimiza ndoto zao.

Mwanjelwa alitoa wito huo jana, alipowatembelea wanafunzi hao katika kambi ya kitaaluma iliyopo Chuo cha Ualimu Bariadi na kuwasisitiza walimu mbali na kuwafundisha masomo ya darasani pia wawafundishe namna ya kukabiliana na maisha baada ya kumaliza masomo ili ambao hawatabahatika kuendelea na masomo ya juu waweze kujiajiri na kuajiri wengine.

Katika hatua nyingine Mwanjelwa amewataka wanafunzi kuitumia fursa ya uwapo wao kambini kufanya kile kilichowapeleka, watumie muda mwingi kujifunza na wajiepusha na mahusiano ya kimapenzi ambayo yatawasababishia kushindwa kutimiza malengo yao ya baadaye.

"Maisha bila malengo sio maisha, angalia nini matarajio yako baada ya kusoma na endepo hautafaulu ujue namna ya kujiajiri, tumieni fursa ya kuwa hapa kuhakikisha mnasoma kwa bidii, ishikeni sana elimu Mungu hatakuacha...maisha lazima myatafute, myatolee jasho," alisema Mwajelwa na kuongeza:

"Wanafunzi wa kike jitunzeni lindeni utu wenu, asitokee mtu akawadanganya mkashindwa kufikia ndoto zenu, ninyi ni wa thamani kubwa kumbukeni mbali na mimba, kuna magonjwa."

Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini, alisema kama mkoa wataendelea kusimamia fedha zote zinazotolewa na serikali za elimu bila malipo ili ziweze kuleta matokeo chanya.

"Tunatamani kuona elimu bure inayotolewa na serikali inazaa matunda, tutapambana kuhakikisha vituo vya kutolea elimu vinakuwa na mazingira bora na kama mlivyomwahidi mhe. (Mwanjelwa) hapa kuwa ziro hakuna na iwe hivyo," alisema Sagini.

# Usafirishaji wa marobota pamba wapata ufumbuzi

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MKURUGENZI wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, amesema shirika hilo limejipanga kuhakikisha linarahisisha huduma za usafirishaji wa marobota ya pamba kwa njia ya reli.

Kadogosa amesema lengo ni kuvipunguzia gharama viwanda vya kuchambua pamba.

Mbali na kupunguza gharama hizo, ameongeza kuwa njia hiyo ni salama na ya uhakika hata kipindi cha mvua mzigo unafika kwa urahisi bila matatizo, huku akibainisha kuwa shirika lake litaweka miundombinu rafiki wakati wa usafirishaji huo.

Kadogosa alisema hayo jana alipotembelea viwanda vya kuchambua pamba vya Alliance kilichopo Kata ya Kasoli na NGS katika Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu na kuongeza kuwa mbali na kusafirisha marobota hayo, wananchi wanapaswa kutumia fursa hiyo kwa kuhakikisha wanabadilisha maisha yao na uchumi kwa ujumla.

Tumejipanga kuweka miundombinu itakayowasaidia mizigo yakiwamo marobota ya pamba kusafirishwa kwa urahisi bila usumbufu, niwaombe wafanyabiashara watumie fursa hii ya reli kufanya shughuli mbalimbali zitakazowaingizia vipato, hivyo kubadilisha maisha yao," alisema Kadogosa.

Aliongeza kuwa ni vyema jamii ione umuhimu wa kujenga viwanda vya nyama ili iweze kusafirishwa nyama badala ya mifugo ambapo Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa wafugaji wakubwa nchini.

Mkuuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema kumekuwapo na changamoto kubwa inayowakabili wafanyabiashara hususan katika usafirishaji wa marobota ya pamba kwani wanalazimika kutumia magari jambo linalopelekea kusafirisha mizigo michache kwa gharama kubwa.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Simiyu, Enock Yakobo, aliwasisitiza wafanyabiashara hao kuona haja ya kutumia reli kwani huduma hiyo imesogezwa karibu na itawasaidia kuepukana na changamoto mbalimbali ikiwamo ya gharama za usafirishaji na potevu wa marobota ya pamba.

Aliongezea kuwa ni vyema ujenzi wa eneo la kuhifadhia marobota ya pamba eneo la Malampaka ukazingatiwa, huku akiongeza kuwa ujio wa usafirishaji wa kupitia njia ya reli utawarahisishia na kuwapunguzia gharama wenye viwanda vya kuchambua pamba.

Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Simiyu, Ibrahim Kadudu, alisema makisio ya mkoa ilikuwa kuzalisha kilogramu milioni 180 na hadi kufikia Septemba 22, mwaka huu, jumla ya pamba kilogramu milioni 148,836,601 zilikusanywa kwenye vyama vya ushirika.

Alisema pamba iliyosafirishwa ni kilogramu milioni 116,391,208, iliyolipiwa kati ya pamba iliyosafirishwa ni kilogramu milioni 85,166,453 , kilogramu milioni 31,106,816 zilisafirishwa bila kulipiwa huku kiasi kilogramu milioni 32,445,393 zikiwa bado kwenye maghala na kwa baadhi ya wakulima.



Mbunge wa Viti Maalum mkoani Shinyanga, Azza Hilali (kushoto), akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, wakigawa msaada wa chakula kwa wazee wanaolelewa katika kambi ya Busanda iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Warundi wahukumiwa kuishi kinyemela

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi, imewahukumu watu wanne raia wa Burundi kulipa faini ya jumla ya Sh. 200,000 au kifungo cha miezi sita kila mmoja, baada ya kupatikana na hatia ya makosa mawili ya kuingia na kuishi nchini bila kibali.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, James Karyamah, kufuatia washtakiwa kukiri makosa bila ya kulazimishwa.

Washtakiwa hao ni Jose Lyne Niyonere (32), Nkindi Tanuy Lionel (27), Retta Mukezamfura (25) na Nkindi Racia Arielia (23) wote kutoka Burundi.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu, Hakimu Karyamah aliwauliza washtakiwa kwa nini wasipewe adhabu kali kutokana na makosa waliyoyafanya, ambapo kila mmoja waliiomba Mahakama iwaonee huruma kwani haikuwa lengo lao kuishi, bali walikuwa wanapita njia kuelekea Msumbiji na baadaye kwenda Ufaransa kutafuta maisha.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Karyamah alimuuliza Mwanasheria wa Serikali iwapo ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa washtakiwa na kueleza hana, hivyo aliwahukumu kila mmoja kulipa faini ya Sh. 500,000, na watakaposhindwa watumikie kifungo cha miezi sita kila mmoja.

Washtakiwa wote wamelilipa faini, hivyo kunusurika kwenda gerezani. Waliwekwa chini ya uangalizi wa Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya kurejeshwa makwao.

Awali ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Juma Maige, kwamba washtakiwa walikamatwa Oktoba 3, mwaka huu majira ya usiku na maofisa wa Idara ya Uhamiaji, katika nyumba moja ya kulala wageni katika Manispaa ya Lindi.

Nipashe
# Spotika



**NYOTA WA3 WATAKAOMPIKU MESSI TUZO YA BALLON D'OR UK. 16 & 17**




## ISIKUPITE

KATIKA mechi ya juzi dhidi ya Brighton, Kipa wa Tottenham, Hugo Lloris alifanyiwa mabadiliko ['subbed'] baada ya dakika ya nane, hivyo kuwa kipa wa kwanza Ligi Kuu England kuweza kufanyiwa mabadiliko mapema zaidi, akivunja rekodi yake mwenyewe dhidi ya Leicester Aprili 2015 (alipofanyiwa 'sab' dakika ya nne).

## BEGA KWA BEGA

Beki wa Leicester City, Caglar Soyuncu, akijaribu kumdhibiti mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah kwa kumvuta mkono baada ya kumzidi ujanja kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi na Liver kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

SOKA




# KWA NINI HAZARD ANATESEKA MADRID?

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard kwa uhakika kabisa alikuwa mchezaji bora wakati akicheza kwenye Ligi Kuu ya England na hivyo kujikuta akiingia kweye rada za kutakiwa Real Madrid.

**Wakati alipowasili Real Madrid kila mmoja alimtarajia kwamba angefanya vizuri. Baada ya yote mambo yalibadilika na kujikuta akiwa na mwanzo mbaya kwa miamba hao wa Hispania.**

Kwa bahati mbaya wengi walikuwa na matarajio naye makubwa, lakini amejikuta ameanza tofauti na matarajio ya wengi na raia huyo wa Ubelgiji amekuwa akihaha kurudi kwenye kiwango chake kama alivyokuwa kule Chelsea, kabla ya juzi, Jumamosi kufanikiwa kuanza kufungua akaunti yake ya mabao kwa kutupia moja wakati wakishinda 4-2 kwenye mechi ya La Liga dhidi ya Granada.

Makala haya yanakuchambulia sababu nne kwa nini nahodha huyo wa timu ya Taifa ya Ubelgiji anateseka sana kule kwenye dimba la Santiago Baranabeu.

**1. KUTOKUWA FITI**

Hazard hajawa fiti vya kutosha kama wachezaji wengi duniani. Hata wakati akiwa pale Chelsea, alikuwa na msimu mmoja au miwili ambayo mwanzoni mwa msimu alikuwa hayupo kwenye kiwango chake. Bahati mbaya, aliwasili pale Real akiwa hayupo kwenye kiwango chake. Zaidi ni kwamba anahitaji muda wa kuzoea maisha na soka la Hispania.

Hazard hatarajiwi kuwa fiti kama Ronaldo, lakini anatakiwa kurudi kwenye kiwango kama kile alichokuwa nacho kipindi akiwa chini ya kocha Antonio Conte. Kama anataka kurudi kwenye kiwango chake ni lazima abadilike haraka.

**2. TIMU MPYA**

Hazard alikuwa akitumika kama ndiye mchezaji muhimu pale Chelsea. Kila kitu kilichokuwa kikifanywa pale Chelsea kilikuwa kinamzunguka yeye. Wachezaji wote walikuwa wakimwangalia Hazard. Hilo halipo pale Madrid.

Hazard hajaonekana kuwa muhimu kikosini hapo na kulazimika kutafuta mpira kwa walinzi. Zaidi ni kwamba Real wanastaili ya kucheza taratibu ambapo Hazard inamwia vigumu kupata mpira. Nyongeza ni kwamba, Hazard harudi nyuma kufuata mpira kama ilivyokuwa pale Chelsea. Staili ya uchezaji ya Real Madrid inamfanya kukaa zaidi mbele na hivyo kutokuwa na nafasi ya kupata mpira. Na kwa kuwa yeye si mzuri kwa kucheza mipira ya vichwa, hawezi kupata mipira mingi kutoka kwa Gareth Bale.

**3. KUTOJIAMINI**

Huwezi kutarajia wachezaji bora duniani kukosa kujiamini, lakini pengine unaweza kushangaa hilo kwa Hazard. Anaichezea klabu ya ndoto zake chini ya mtu aliyekuwa akimvutia zaidi. Pengine anaweza kuwa na woga na angependa kuwatuliza wachezaji wenzake. Hilo pengine linaweza kuwa tatizo la kuwafanya wachezaji wenzake kuwa na muda mwingi wa kucheza mpira. Lakini woga mwingine pengine ni sababu anacheza katika klabu kubwa ambayo aliiota kwa miaka mingi na hivyo kumfanya kucheza kwa kutojiamini kama yupo ndani ya kikosi hicho.

**4. SIKU ZA MWANZO**

Huku vyombo vya habari vikizungumza mno kuhusu namna Hazard alivyotua pale Real Madrid, cha kuzingatia hapa ni kwamba hizi bado ni siku za mwanzo kabisa kwa Hazard. Hata kwa mchezaji kama Luka Modric ilimchukua zaidi ya mwaka kuweza kung'ara katika kikosi cha Madrid.

Hazard ni aina ya mchezaji ambaye anatarajiwa kusukumiza mashambulizi mbele, kwani uchezaji wake ni wa kusubiri zaidi mipira kutoka winga na kuja mbele. Hivyo, kwa kuwa hizi ni siku zake za mwanzo kuna uwezekano akapata nafasi ya kujiimarisha zaidi siku za mbeleni na kurudi kwenye kiwango chake.

Baada ya muda anaweza kuanza kuzoea staili na uchezaji wa Real Madrid na kile ambacho wengine wanakitarajia kutoka kwake, hivyo ni suala la muda tu.

**JE, WAJUA?**

KATIKA mechi ya juzi dhidi ya Leicester City, Sadio Mane, ametimiza mechi ya 100 na mabao 50 kwenye ligi akiichezea Liverpool, hivyo kuwa mchezaji wa 10 katika historia ya klabu hiyo kuweza kufikisha idadi hiyo ya mechi na mabao.

MICHEZO




Straika wa Simba Meddie Kagere (kulia), akishangilia bao na wachezaji wenzake, baada ya kufunga kwa mkwaju wa penalti dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba na kuipa timu yake ushindi wa mabao 3-0.

# PENALTI ZILIVYOADIMIKA LIGI KUU BARA 2019/20

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara inamaliza raundi ya tano, ni penalti mbili tu zimepatikana mpaka sasa na kuweka rekodi ya kupatikana penalti chache zaidi tofauti na msimu uliopita hadi kufikia raundi hiyo tayari jumla ya penalti saba zilikuwa zimeshapatikana na zote kuwekwa wavuni.

**Kabla ya mechi ya jana Jumapili kati ya Yanga dhidi ya Coastal Union, penalti mbili tu zilikuwa zimepatikana hadi kufikia raundi ya tano, kwa michezo 43 ambayo ilikuwa imeshachezwa.**

Penalti zilizokuwa zimepatikana kabla ya mechi ya jana ni ile ya Septemba 26 kati ya Kagera Sugar dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Kaitaba.

Ilikuwa ni penalti ya kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu ilipatikana kwenye raundi ya nne na iliwekwa wavuni na Meddie Kagere wa Simba, akiibeba timu yake kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar.

Penalti nyingine ilipatikana siku tatu baadaye Septemba 29, kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, kati ya KMC dhidi ya Ndanda FC ikiwa ni mechi ya raundi ya tano.

Ally Ramadhani aliifungia KMC bao kwa mkwaju huo na kuifanya timu yake kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ndanda. Hii ni idadi ndogo zaidi kupatikana tofauti na msimu uliopita ambapo hadi kufikia raundi ya tano na mechi 46 kuchezwa tayari zilikuwa zimepatikana penalti saba na zote zikatendewa haki.

**PENALTI SABA ZA MSIMU ULIOPITA**

Mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu msimu uliopita 2018/19, ilipatikana penalti ya kwanza kwenye mechi kati ya Yanga dhidi ya Mtibwa Sugar Agosti 23 kwenye Uwanja wa Uhuru.

Kwenye mechi hiyo ambayo Yanga ilishinda mabao 2-1, penalti ilipatikana kwa upande wa Yanga na Kelvin Yondani akaitendea haki.

Raundi ya pili zilipatikana penalti mbili kwenye mechi kati ya Stand United dhidi ya Mbao FC Agosti 25, 2018. Stand ilikufa nyumbani mabao 2-1, la pili likiwa la penalti iliyowekwa nyavuni na Said Hamisi.

Kwenye raundi hiyo hiyo Agosti 27, mwaka jana, Azam nayo ilibahatika kupata penalti kwenye uwanja wake wa nyumbani na kuwekwa wavuni na Tafazwa Kutinyu ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Ndanda FC.

Raundi ya nne pia zilipatikana penalti mbili, moja kwenye mechi kati ya Prisons na Ruvu Shooting mjini Mbeya ambapo timu hizo zilitoka sare mabao 2-2, la kusawazisha la Ruvu likifungwa na Hamisi Mcha kwa tuta. Hiyo ilikuwa ni Septemba 14, 2018.

Siku hiyo hiyo, Mbao nayo ikafa nyumbani CCM Kirumba kwa bao 1-0 la mkwaju wa penalti iliyofungwa na Ally Ahmed Shiboli. Ilipofika raundi ya tano, zikapatikana pia penalti mbili na kuhitimisha jumla ya penalti saba.

Mbeya City ikiwa nyumbani Septemba 14, mwaka jana iliichapa Ruvu Shooting mabao 4-3. Moja ya bao la Ruvu Shooting lilikuwa la penalti ambayo ilifungwa na Hamisi Mcha.

Ilikuwa ni mechi iliyochezwa Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza, Mbao ilipoiadhiri Simba bao 1-0 Septemba 20, 2018 likiwa ni la mkwaju wa penalti likifungwa na Said Hamisi.

**MABAO YA KUJIFUNGA**

Mpaka sasa ni wachezaji watatu wamejifunga wenyewe kwenye Ligi Kuu inayoendelea ambayo ipo kwenye raundi ya tano.

Ibrahim Said wa Mbao, alijifunga kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Alliance na kusababisha ikose ushindi, badala yake ikatoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza.

George Chota, mchezaji wa Mbeya City, yeye alijifunga kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Ruvu Shooting. Bao lake hilo liliinyima ushindi timu yake na kuisawazishia Ruvu ikatoka sare ya bao 1-1.

Mchezaji wa Polisi Tanzania, Yassin Mustapha alijifunga kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting na kuipa timu pinzani ushindi wa bao 1-0.

**NJE YA UWANJA**

KADI nyekundu aliyozawadiwa beki wa pembeni wa Everton, Seamus Coleman, kwenye mechi dhidi ya Burnley, ni ya pili kwake kwenye Ligi Kuu England na ikifanya sasa tangu kuanza kwa msimu uliopita, wachezaji wa Everton kuzawadiwa jumla ya kadi nyekundu sita kwenye ligi hiyo, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuliko timu nyingine.



## Extra Time

# NYOTA WA3 WATAKA-OMPIKU MESSI TUZO YA BALLON D'OR




VAN DIJK

RONALDO

**BARCELONA,** Hispania

TUNAELEKEA mwishoni mwa mwaka huu na ushindani wa kuwania tuzo ya Ballon d'Or tayari upo juu. Kuna wachezaji wengi ambao wana ndoto ya kuibeba tuzo hii siku moja.

**Lionel Messi hivi karibuni alishinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa.**

Kwa upande mmoja inaonekana kwamba, kushinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Fifa ni kama tiketi ya kushinda tuzo ya Ballon d'Or ambapo kama Messi ataitwaa itakuwa ni kwa mara ya sita katika historia.

Na ukiangalia kiwango alichokionyesha msimu uliopita ni sawa kabisa kwa nyota huyo wa kimataifa wa Argentina kuitwaa tuzo hiyo.

Pamoja na yote hapa tunawaangalia wachezaji watatu ambao wanaweza kumpiku Messi kutwaa tuzo hiyo msimu huu ambapo itatolewa Desemba mwaka huu:

### 3. MOHAMED SALAH

Mchezaji pekee kutoka bara la Afrika ambaye yupo kwenye orodha ya wanaowania ni mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah. Alikuwa na msimu bora uliopita kwa kuiwezesha Liverpool kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Raia huyo wa Misri alikuwa na mchago mkubwa zaidi kwa kikosi cha kocha, Jurgen Klopp katika mbio za ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na walimaliza nafasi ya pili kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England.

Salah pia alimaliza akiwa mmoja wafungaji bora wa Ligi Kuu ya England na kushinda tuzo ya Kiatu cha Dhahabu pamoja na Pierre-Emerick Aubameyang na Sadio Mane ambapo wote kila mmoja alifunga mabao 22.

Ingawa Liverpool ilipitwa kwa pointi moja tu katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu uliobebwa na Manchester City, Salah ana nafasi kubwa ya kuibeba tuzo hiyo. alifunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho mbili katika michuano hiyo na hivyo ana nafasi kubwa ya kumpiku Lionel Messi mwaka huu.

### 2. CRISTIANO RONALDO

Kuna mashabiki wengi wa soka ambao watakubaliana na ukweli kwamba, mchezaji huyu wa kimataifa wa Ulaya ana nafasi ya kumpiku Messi katika mbio za kuwania tuzo ya Ballon d'Or mwaka huu.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 34, alishinda tuzo ya mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi katika Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu uliopita baada ya kutikisa nyavu mara 21 na kutengeneza pasi za mwisho nane katika mechi 31 za ligi hiyo. Pia alishinda tuzo ya mfungaji bora wa Ligi ya Mataifa ya Uefa na alikuwa na mchango mkubwa wa kutwaa taji la mashindano hayo.

Akiwa na klabu ya Juventus, raia huyo wa Ureno alishinda taji la Serie A na lile la Supercoppa d'Italiano. Pia alifunga mabao mengi pamoja na 'hat-trick' dhidi ya Atletico Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hivyo Ronaldo bado ana nafasi kubwa ya kumpiku Messi kwenye mbio za kutwaa tuzo hiyo.

### 1. VIRGIL VAN DIJK

Beki huyu ni mmoja wa wachezaji ambaye anapewa nafasi kubwa zaidi kutokana na kiwango alichokionyesha msimu uliopita. Raia huyu wa Uholanzi alikuwa katikati ya mafanikio ya Liverpool kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na nafasi kubwa ya kumpiku Messi.

Alikuwa kuwa sehemu kubwa ya mafanikio ya Liverpool pia kwenye mbio za kuwania ubinga wa Ligi Kuu ya England, wakipitwa pointi moja na Man City. Kwa sasa beki huyo tayari ana taji, kwani alilileba lile la Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na kuisaidia Uholanzi kucheza fainali ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, ambapo alifungwa na Ureno ya Ronaldo.

Van Dijk alimaliza nafasi ya pili nyuma ya Messi kwenye tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Fifa hivi karibuni na tayari ameshashinda tuzo ya mchezaji bora wa Ulaya, hivyo ana nafasi kubwa ya kumpiku Messi na kuibeba tuzo ya Ballon d'Or.

## Nukuu

"Kama nikikaa baa, linaonekana kama wazo zuri kwa upande wangu. Lakini kama nikiwa kwenye benchi, natakiwa kuangalia uwiano wa timu, endapo timu baadaye itakuwa kwenye uwiano mzuri, tunaweza kujaribu, lakini kwa sasa bado haijakaa sawa," **Kocha wa Juventus, Maurizio Sarri akieleza namna ambavyo hashawishika na wazo la kuwaanzisha pamoja kwenye safu ya ushambuliaji, Cristiano Ronaldo, Gonzalo Higuain na Paulo Dybala.**



"Ni vigumu kuzungumza kwa sasa. Sikuwaambia chochote wachezaji baada ya mchezo, tunatakiwa kukaa pamoja, lakini unaweza kuona hatuzungumzi kwa sasa, katika hali hii unatakiwa kuwa kimya na kutulia, baadaye tutazungumza, lakini kwa sasa utulivu ndio unaohitajika. Huu utakwenda kuwa msimu mgumu," **Kocha Mauricio Pochettino baada ya Tottenham kuchezea kichapo cha mabao 7-2 dhidi ya Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.**



"Ndio tumewapoteza Alexis na Romelu, tunahitaji mshambuliaji mbunifu mwenye kiwango bora cha kufunga mabao, naamini kwamba, dirisha la usajili la Januari utakuwa wakati mzuri kwa upande wetu kutafuta mshambuliaji ambaye ataweza kuongeza nguvu kwenye kikosi chetu. Kwa sasa bado tuna tatizo la ufungaji, ingawa nina wachezaji vijana, bado hawana uzoefu wa kutosha, hivyo ni lazima tutafute mshambuliaji mpya kwa ajili ya kuwa na nafasi ya kuweza kufunga," **Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer**





Beki wa Yanga, Lamine Moro (kushoto), akitafuta mbinu za kumkaba straika wa Polisi Tanzania, Ditram Nchimbi aliyewafunga hat-trick Alhamisi iliyopita.

# NCHIMBI NA MAAJABU YA HAT-TRICK ZA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Polisi Tanzania, Ditram Nchimbi, Alhamisi iliyopita aliweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kwenye Ligi Kuu ya Tanzania kufunga mabao matatu kwenye mechi moja 'hat-trick' katika mchezo dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**Nchimbi, anayeichezea Polisi Tanzania kwa mkopo akitokea Azam, alifunga mabao hayo dakika ya 33, 55 na 57 na kuifanya timu yake kutoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Yanga.**

Mabao ya Yanga yalifungwa na Mrisho Ngassa na David Molinga aliyefunga mawili.

Hivyo, Nchimbi amekuwa Mtanzania wa kwanza kufunga 'hat-trick', baada ya misimu miwili ya utawala wa wachezaji kutoka nje ya nchi kuwa wa kwanza kufanya hivyo.

"Najisikia furaha ambayo siwezi kuelezea. Ilikuwa ni ndoto yangu kila siku nikiwaza kuwa kuna siku nifunge na mimi 'hat-trick', kwa bahati nzuri leo nimeipata, tena kwa kuifunga timu kubwa kama Yanga ni furaha sana." Anasema Nchimbi ambaye siku moja tu baadaye akaitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars ambacho kwa mujibu wa wachambuzi wa masuala ya soka kina tatizo kwenye safu ya ushambuliaji.

"Nafunga mabao haya siyo kushindana na mtu, ila nafanya hivi kwa kuisaidia timu yangu ya Polisi. Wala kichwani kwangu sina wazo la kutaka kuwa mfungaji bora na kuchukua Kiatu cha Dhahabu, lakini kama ikitokea hivyo nitafurahi," anasema mchezaji huyo.

Mara ya mwisho Mbongo kuwa wa kwanza kupiga 'hat-trick' kwenye Ligi Kuu ilikuwa ni msimu wa 2016/17, wakati Kelvin Sabato alipokuwa akichezea Mtibwa Sugar alipofanya hivyo dakika ya pili, 35 na 64, timu yake ikitoka sare nyumbani dhidi ya Stand United.

Baada ya hapo, ukaja utawala na wachezaji wa kigeni kwani msimu wa 2017/19, Mganda Emmanuel Okwi wa Simba alipiga 'hat-trick' ya kwanza kwenye Ligi Kuu kwenye mechi ya ufunguzi wa ligi, Simba ikishinda mabao 7-0 dhidi ya Ruvu Shooting Uwanja wa Uhuru.

Msimu uliopita 2018/19, Mrundi Alex Kitenge alikuwa wa kwanza kufunga 'hat-trick' alipofanya hivyo kwenye mechi dhidi ya Yanga Uwanja wa Taifa, Yanga ikishinda mabao 4-3 kwenye Uwanja wa Taifa.

**YANGA MISIMU MIWILI MFULULIZO**

Yanga imejiwekea rekodi mbaya kwenye Ligi Kuu, kwani imefungwa 'hat-trick' kwa misimu miwili mfululizo, tena zikiwa ni za kwanza za msimu.

Msimu uliopita, Septemba 16, mwaka jana, Kitenge alipata 'hat-trick' akiifunga Yanga dakika ya 14, 58 na 90 ikiwa ni ya kwanza ya msimu na msimu huu, Oktoba 3, Yanga iliruhusu tena hat-trick ikiwa ni ya kwanza ya msimu, safari hii ikifungwa na Nchimbi ambaye ni straika wa zamani wa timu za Njombe Mji, Majimaji, Mbeya City na Mwadui FC.

**MOJA KIPINDI CHA KWANZA**

Mabao yote ya hat-trick ambayo Yanga imefungwa kwa misimu miwili mfululizo ni kwamba wafungaji wanapata bao moja kipindi cha kwanza na kipindi cha pili wanafunga mawili.

Ukiangalia dakika ni kwamba Kitenge alifunga dakika ya 14, mawili kipindi cha pili dakika ya 58 na 90 na ile ya Nchimbi ni dakika ya 33 kipindi cha kwanza na mengine kipindi cha pili dakika ya 55 na 57.

**NGASSA AKIFUNGA NI HATARI**

Hii ni rekodi mbaya kwa Ngassa, kwani inaonekana kuwa akianza kuifungia Yanga bao dakika za mwanzo, basi kuna hatari mchezaji wa timu pinzani kufunga hat-trick.

Kwenye mechi ya Alhamisi iliyopita, winga huyo alifunga bao dakika ya tano, lakini dakika 90 zilipomalizika, mchezaji wa timu pinzani ya Polisi Tanzania alifungwa hat-trick na timu hizo kutoka sare ya mabao 3-3.

Msimu uliopita, Ngassa alifunga bao dakika ya kwanza ya mchezo dhidi ya Stand United, kilichotokea ni kwamba mchezaji wa upande wa pili, alifunga hat-trick na mechi hiyo kumalizika kwa Yanga kushinda mabao 4-3.

Mabao mengine ya Yanga yalifungwa na Ibrahim Ajibu ambaye kwa sasa amerejea kwenye klabu yake ya zamani ya Simba, Andrew Vicent 'Dante' ambaye kwa sasa ameiwekea mgomo timu yake hiyo akishinikiza kulipwa madai yake, na Deus Kaseke ambaye alikuwapo kwenye mechi ya Alhamisi iliyopita na aliingia kipindi cha pili cha mchezo huo.

**NAJUA WAJUA**

PREMIER LEAGUE

NORWICH (mashuti 21) vs Aston Villa (mashuti 22), imekuwa mechi ya kwanza Ligi Kuu England kushuhudiwa timu zote zikipiga takriban mashuti 20 kila moja tangu mechi dhidi ya QPR (24) vs Swansea (25) Januari 2015.

## SOKA

# PUKKI: MKALI NYAVUNI ANAYEVIZIA KIATU EPL



**LONDON,** England

WAKATI Ligi Kuu ya England ikianza, hakuna aliyetarajia kuliona jina la Teemu Pukki katika orodha ya wafungaji wanaoongoza kwa kuzifumania nyavu. Huyu ni mshambuliaji wa Klabu ya Norwich City.

**Ni raia wa Finland nchi ambayo haina historia kubwa ya kutoa wachezaji wenye majina makubwa duniani.**

Juni 30, mwaka jana, Pukki alijiunga katika klabu ya Daraja la Kwanza ya Norwich City akiwa mchezaji huru huku akisaini mkataba wa miaka mitatu.

Alicheza mechi ya kwanza Agosti 4 katika sare ya 2-2 dhidi ya Birmingham City. Wiki moja baadaye akafunga bao lake la kwanza katika kichapo cha mabao 4-3 nyumbani dhidi ya West Bromwich Albion.

Kuanzia Januari hadi Februari 2019, Pukki alifunga mabao nane katika mechi sita mfululizo ikiwamo mabao mawili aliyofunga katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Bolton Wanderers. Pia alifunga mabao mawili katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Ipswich Town mnamo Februari 10.

Kwa kufunga mabao hayo alikuwa mchezaji wa Finland aliyefunga mabao mengi zaidi katika historia ya Ligi Daraja la Kwanza akimpiku staa wa zamani wa Ipswich Shefki Kuqi.

**ALIKOTOKA**

Licha ya kukipiga pia timu ya Taifa ya Finland, msimu huu Pukki alianza kwa kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu mnamo Julai 3, mwaka huu. Agosti 9 alifunga bao lake la kwanza la Ligi Kuu huku Norwich wakichapwa 4-1 ugenini kwa Liverpool. Siku nane baadaye akapiga hat-trick katika pambano dhidi ya Newcastle wakishinda 3-1.

Hatimaye Pukki alinunuliwa na Sevilla ya Hispania akitokea KTP na alijumuishwa katika mechi ya kwanza katika mechi ya ugenini dhidi ya Real Madrid Desemba 7, 2008. Aliishia benchi. Alicheza mechi ya kwanza Januari 25, 2009 katika mchezo dhidi ya Racing. Baadaye aliishia kucheza timu ya akiba na mwisho alirudi kwao Finland.

Agosti 28, 2010 Pukki alisaini mkataba wa miaka mitatu na nusu na klabu ya HJK Helsinki ya Finland. Mwaka 2011 alifunga mabao 11, huku akitengeneza mengine nane katika mechi 18 za ligi.

Alichaguliwa katika timu ya msimu ya Ligi ya Finland. Alikuwa mchezaji muhimu katika kikosi cha HJK Helsinki ambacho kilishiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa na kisha Europa.

Alifunga mabao mawili dhidi ya Bangor City katika ushindi wa mabao 2-0, lakini pia akafunga mabao mawili katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Schalke nyumbani. Akafunga bao pekee katika kichapo kikali cha mabao 6-1 walicholambwa ugenini na Schalke.

Kutokana na mabao yake hayo matatu dhidi ya Schalke klabu hiyo ya Ujerumani iliamua kumnasa Agosti 31, 2011 akisaini mkataba wa miaka mitatu. Novemba 6, alifunga mabao mawili katika pambano lake la kwanza dhidi ya Hannover 96.

Kwa kufunga mabao hayo mawili alikuwa mchezaji wa tatu wa Finland katika historia ya Bundesliga kufunga mabao mawili ndani ya mechi moja. Wengine waliowahi kufanya hivyo hapo awali ni Ari Hjelm na Pasi Rautiainen.

Agosti 31, 2013, Pukki alitua katika klabu ya Celtic ya Uskochi kwa dau ambalo halikutajwa. Alifunga bao katika mechi yake ya kwanza tu dhidi ya Hearts mnamo Septemba, 14, 2013. Akafunga tena katika mchezo uliofuatia dhidi ya St Johnstone Septemba 21. Januari 26, 2014 akafunga dhidi ya Hibernian.


Julai 8, 2014 akaifungia Celtic hat trick katika mchezo wa maandalizi ya msimu dhidi ya LASK Linz ambapo walishinda 5-2. Akafunga mabao mawili katika mechi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa wa Ulaya dhidi ya KR Reykjavik. Hata hivyo baadaye akajikuta ameshuka kiwango chake klabuni hapo.

Septemba Mosi 2014 baada ya kuchemsha na Celtic, Pukki alisaini mkataba wa mkopo wa mwaka mmoja katika klabu ya Brøndby IF ya Denmark huku klabu hiyo ikipewa fursa ya kumchukua jumla mwishoni mwa msimu.

Alimaliza msimu akiwa mfungaji bora wa klabu akifunga mabao tisa. Juni 19, 2015, Pukki alisaini mkataba wa miaka mitatu kukipiga Brøndby. Julai 31, 2017 alifunga bao moja dhidi ya VPS katika mchezo wa kwanza wa kufuzu michuano ya Europa 2017-18 huku Brøndby wakishinda 2-0. Mei 10, 2018 alicheza mchezo wa fainali wa Kombe la Denmark wakishinda 3-1 dhidi ya Silkeborg IF.

Mwishoni mwa msimu wa 2017-18 aliachwa bure baada ya kushindwa kukubaliana dili jipya na klabu hiyo na ndipo akatua Norwich City.

KIPIGO cha mabao 5-1 ilichokitoa Aston Villa dhidi ya Norwich juzi, kinaifanya kuwa klabu ya kwanza iliyopanda daraja kuweza kupata ushindi mkubwa kama huo ugenini kwenye Ligi Kuu England tangu Bolton ilipofanya hivyo nyumbani kwa Leicester Agosti mwaka 2001.



NDANI YA 18



TUNAELEKEA mwishoni mwa mwaka huu na ushindani wa kuwania tuzo ya Ballon d'Or tayari upo juu. Kuna wachezaji wengi ambao wana ndoto ya kuibeba tuzo hii siku moja.

Uk. 16&17



MILAN SKRINIAR

# MABEKI WA KATI WATATU WATAKAOMFAA GUARDIOLA

**MANCHESTER,** England

NI mechi nane tu za Ligi kuu England zilizochezwa hadi sasa na Manchester City tayari inakumbwa na matatizo katika safu yake ya mabeki wanne.

**Washindi hao wa mataji manne msimu uliopita ambao kwa sasa wapo nafasi ya pili nyuma ya Liverpool kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, tayari wamewapoteza walinzi wao wa kati wawili muhimu kutokana na majeraha.**

Beki wa Hispania, Aymeric Laporte amefanyiwa upasuaji wa goti baada ya kuumia wakati City wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Brighton, ambapo John Stones aliumia misuli na bado hajapona hadi sasa na anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa muda.

Wakati kocha wa City, Pep Guardiola akiwa amekumbwa na matatizo hayo kwenye safu ya ulinzi amemfanya kiungo, Fernandinho kuziba nafasi ya Laporte na Stones kwenye kikosi cha kwanza kwa kumchezesha kama beki wa kati.

Tangu Laporte na Stones wakiwa majeruhi, kikosi hicho cha Guardiola kimepoteza mchezo muhimu dhidi ya Norwich na matatizo kwenye safu ya ulinzi yakiendelea kumpa wakati mgumu.

Kikosi kina wachezaji ambao wanaweza kuziba mapengo mengine kama Nicolas Otamendi ambaye ana thamani ya kikosi cha kwanza, lakini ushindani wa Ligi Kuu ya England ni mgumu na hivyo, lazima watafute wanaoweza kuziba kabisa mapengo hayo.

Hivyo, Man City kwa vyovyote ni lazima waingine sokoni wakati wa kipindi cha usajili wa dirisha dogo Januari ili kuimarisha kikosi chake.

Hapa tunawaangalia mabeki wa kati watatu ambao Guardiola atatakiwa kuwaangalia katika usajili wake wa dirisha dogo la Januari kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake, twende...

**3. JOSE GIMENEZ (ATLETICO MADRID)**

Mmoja wa mabeki wanaochukuliwa kwamba wapo kwenye kiwango cha juu zaidi barani Ulaya kwa sasa ni Jose Gimenez wa Ateltico Madrid. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay amekuwa mmoja wa mabeki bora zaidi Ulaya kwa kipindi cha miaka minne iliyopita pamoja na timu yake ya taifa.

Akiwa ana umri wa miaka 24, Gimenez anaweza kuwa suluhisho bora zaidi kwa Guardiola na Manchester City wakiwa wanatafuta beki ambaye atakaa na kikosi hicho kwa muda mrefu.

Gimenez ana ubora wote unaomfanya kuwa beki bora kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya England na ana nafasi nzuri ya kuweza kuisaidia timu hiyo. Gimenez anaweza kuwagharimu Man City euro milioni 70.

**2. ALESSIO ROMAGNOLI (AC MILAN)**

Kihistoria walinzi wa Italia wanachukuliwa kwamba ndio wenye mbinu na ujuzi mzuri zaidi barani Ulaya. Na mmoja wa mabeki hao wa Italia kwa sasa ambaye yupo kwenye kiwango cha juu ni mlinzi wa AC Milan, Alessio Romagnoli.

Beki huyo wa kati amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa za Ulaya pamoja na zile za Ulaya kwa muda wa miaka kadhaa. Romagnoli anachukuliwa kuwa ndiye Giorgio Chiellini ajaye kwa kikosi cha timu ya Taifa ya Italia hasa kutokana na uwezo wake dimbani wa kuongoza safu ya ulinzi.

Katika umri wake wa miaka 24, atakuwa chaguo sahihi kwa Manchester City hasa kutokana na falsafa ya klabu hiyo ya kupenda kuwatumia wachezaji vijana.

Muitaliano huyo baada ya kung'ara katika Klabu za Roma na Sampdoria haraka amekuwa na jina kubwa Ulaya na sasa yupo kwenye rada za Pep Guardiola ambaye anapanga kuimarisha safu yake ya ulinzi. Romagnoli ana thamani ya euro milioni 50.

**1. MILAN SKRINIAR (INTER MILAN)**

Beki wa kati wa kimataifa wa Slovakia, Milan Skriniar jina lake limekuwa likitajwa zaidi wakati wa kipindi cha usajili mwaka huu.

Katika orodha ya mabeki waliokuwa wakiwindwa zaidi wakati wa kipindi cha majira ya joto, jina la Skriniar lilishika nafasi ya pili nyuma ya Romagnoli na huku wote wakiwa na umri wa miaka 24 na wote walicheza pamoja kule Sampdoria, na sasa pia wanacheza pamoja pale jijini Milan katika klabu mbili pinzani.

Beki huyu wa Inter ana uwezo mzuri wa kukaba na pia kusukumiza mashambulizi kutokea nyuma, kitu ambacho kitakuwa msaada mkubwa kwa kikosi cha Guardiola na iwapo atampata atakuwa msaada mkubwa zaidi kwa kikosi cha Manchester.

Skriniar pia ana uwezo mkubwa wa kupiga pasi fupi na pia atakuwa patina mzuri wa Rodri ambaye ni usajili mpya pale Man City.

Na kwa pamoja wataweza kuimarisha vizuri zaidi safu ya ulinzi ya Man City kwa kipindi kirefu wakiwa pamoja.

Maofisa wa pale kwenye dimba la Etihad watalazimika kuvunja benki kwa ajili ya kumsajili Skriniar ambaye anatajwa kuwa na thamani ya euro milioni 60, ingawa kocha mpya wa Inter, Antonio Conte amekuwa akimtegemea zaidi mchezaji huyo kwenye kikosi chake.

**USILOLIJUA**



Liverpool ni timu ya kwanza Ligi Kuu England kushinda kwa mara ya pili mechi nane mfululizo za mwanzo wa msimu, pia iliweza kufanya hivyo msimu wa 1990-91.





# Wakulima kujikita kwenye parachichi

**Na Grace Mwakalinga,** ILEJE

WAKULIMA 1,800 katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje mkoani Songwe wamejitosa kulima maparachichi vikonyo kutokana na faida kubwa inayoelezwa kuwa iko ndani ya zao hilo.

Walitangaza uamuzi huo jana, wakati wa kikao cha kujadili mikakati ya namna ya kunufaika na zao hilo. Wakulima wa zao hilo ambalo limetajwa kuwa dhahabu ya ardhini kwa sasa kutokana na faida zinazopatikana, walikuwa kwenye mkutano huo ulioandaliwa na kampuni ya Agri Organic Tanzania.

Walisema wamejihusisha na kilimo cha mazao mengine lakini sasa wameamua kujikita kwenye maparachichi vikonyo kwa sababu kuna faida kubwa ukilinganisha na mazao mengine.

Mmoja wa wakulima hao, Endson Tete alisema kwa miaka 55 sasa amekuwa akijihusisha na kilimo bila faida yeyote lakini ujio wa parachichi vikonyo utawaongezea kipato kama ilivyotokea kwa wakulima wa Rungwe.

"Tuko tayari sasa kujikita kwenye kilimo cha parachichi vikonyo kwa sababu tumeona wenzetu wa Rungwe wanatajirika, tumechelewa kwa sababu ya uzembe wetu maana maeneo ya kulima tunayo ndiko yanakostahili," alisema Tete.

Mwenyekiti wa kikundi cha wakulima Kijiji cha Bwenda, Asubile Atson, alisema walianza kupanda miche ya parachichi vikonyo kwa ajili ya biashara ya zao hilo. Alisema kikundi chake chenye wanachama 20 kimepanda miche 6,165 na kila mche mmoja wanauuza kati ya Sh. 2,500 hadi Sh. 3,000.

Aliongeza kuwa hata hivyo, hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo hicho hivyo wanahitaji wataalamu wasaidie kuongeza tija ya uzalishaji. Mkurugenzi Mtendaji wa Agri Organic Tanzania, Ahadi Mtweve, alisema lengo lao ni kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Ileje wanalima parachichi vikonyo.

Alisema tayari uongozi wa wilaya umetoa baraka kwa kampuni hiyo kuhamasisha kilimo cha parachichi kinafanyika ili liwe zao la biashara kuliko mengine ambayo hayawapatii faida ya kutosha wakulima hao.

Alisema matarajio yao kwa muda wa miaka mitano ni kuhakikisha kilimo cha zao la parachichi vikonyo linabadilisha maisha ya wananchi wa Ileje ambao wamebarikiwa kuwa eneo kubwa la ardhi. "Tunawahakikishia wakulima wa Ileje kupitia kilimo cha parachichi watabadili maisha yao kwa sababu ni zao linalowaingizia fedha nyingi ukilinganisha na mengine kwani ndani ya miaka mitatu mkulima anaanza kuvuna matunda," alisema Mtweve.

Mtaalamu wa masuala ya lishe kutoka Shirika la Feed The Future linalosimamia mradi wa mboga na matunda, Itika Kisunga, aliwahakikisha wakulima wa Ileje kupatiwa baadhi ya vifaa vya kuzalisha miche katika zao la parachichi.

Aidha, aliwafahamisha wakulima kuwa wataendelea kushirikiana na kampuni ya Agri Organic Tanzania, kuhakikisha kinamama na vijana wananufaika na mradi wa mboga na matunda wilayani Ileje. Alisisitiza kuwa mradi wao wa mboga na matunda ni kuwafikia kinamama wengi zaidi kuliko wanaume kwani wao ndiyo wazalishaji wakuu licha ya kutopewa kipaumbele ndani ya familia na jamii kwa ujumla.

"Lengo la mradi wetu wa mboga na matunda ni kuwafikia kinamama zaidi kwani ndiyo maana sehemu kubwa ya kukuza uchumi, lakini pia tunawalenga vijana ili waache kukimbilia mjini wakikwepa shughuli za kilimo vijini. Wanaondoka na kuwaachia wazee ambao hawana uwezo wala nguvu za kutosha kuzalisha," alisema Kisunga.



Wakulima wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje katika Mkoa wa Songwe, wakisikiliza kwa makini maelekezo kutoka kwa wataalamu wa Shirika la Agri Organic Tanzania Limited (hawapo pichani) kuhusu uanzishwaji wa kilimo cha zao la parachichi vikonyo ambalo linatajwa kuwa dhahabu ya ardhini kwa sasa. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wajitosa usafi wa Mto Nzovu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Bonde la Maji la Ziwa Rukwa kwa kushirikiana na uongozi wa sekondari na shule za msingi 13 za jijini Mbeya wameanzisha kampeni maalum ya kusafisha vyanzo vya maji.

Wadau hao wanasafisha vyanzo vya maji ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa maji unaosababishwa na shughuli mbalimbali za uzalishaji.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa, Grace Chitanda, wakati wa mahojiano maalum na Nipashe namna walivyojiandaa kukabiliana na uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji kuelekea msimu wa masika.

Alisema katika kukabiliana na changamoto ya uharibifu wa vyanzo vya maji wameanzisha kampeni ya kufanya usafi kuzunguka vyanzo hivyo, huku wakitoa elimu kwa jamii kuachana na tabia ya kuharibu mazingira.

"Kampeni yetu ya usafi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji tutaifanya kwenye bonde la Mto Zovwe ambalo humwaga maji yake Ziwa Rukwa kwa sababu bonde hilo sasa limevamiwa na shughuli za binadamu ikiwamo utupaji wa taka na mizoga," alisema Chitanda.

Aliongeza kuwa changamoto ya uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji hususani utupaji wa mifuko ya plastiki imechangia kwa kiasi kikubwa upotevu wa viumbe hai katika mito na vyanzo vingine.

Mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Utengule, Valeria Angumbwike, aliomba serikali kuziwezesha shule kutengeneza vyama vya mazingira ili kukabiliana na uchafuzi wa mazingira kwenye vyanzo vya maji. Alisema vyama hivyo vitajikita kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na umuhimu wa kutunza mazingira katika vyanzo

# Madereva waomba elimu ya ebola

**Na Grace Mwakalinga,** TUNDUMA

MADEREVA katika Mji wa Tunduma uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Momba mkoani Songwe wameiomba serikali kutoa elimu ya kutosha kuhusu ebola ili wachukue tahadhari mapema.

Waliiomba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoa elimu juu ya ugonjwa huo hasa maeneo ya mipakani wachukue tahadhari mapema.

Walitoa ombi hilo juzi walipokuwa wakizungumza na Nipashe namna wanavyojitahidi kukabiliana na ebola wanapotoa huduma mpakani.

Madereva hao wanafanya shughuli zao mpakani kwenye watu mbalimbali wakiwamo wageni.

Walisema hawana elimu ya kutosha kukabiliana na ugonjwa huo mbali na maelekezo ya Wizara ya Afya na baadhi ya vipeperushi vinavyosambazwa kutoa elimu na tahadhari.

Miongoni mwa madereva hao, Patrick Eliah alisema hafahamu dalili za ugonjwa huo, lakini anazo taarifa kuwa ugonjwa huo mara nyingi hutokea kwenye mipaka ya nchi.

Aliishauri wizara kuandaa utaratibu wa kuwaelimisha viongozi wa mitaa na vijiji athari za ugonjwa huo ili elimu hiyo iwe rahisi kuwafikia wao.

"Licha ya serikali kutoa tahadhari mipakani na kuandaa wataalamu pamoja na vifaa, lakini makundi kama ya madereva bodaboda ni muhimu yakapatiwa elimu hii.

Mfano sisi wa hapa Tunduma mara nyingi tunabeba abiria kutoka Zambia au Congo hivyo tukipewa tahadhari ya namna ya kujikinga itatusaidia kujinusuru," alisema Eliyah.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Mpakani, Emmanuel Kalekayo, alisema wataalamu na vifaa vya kutosha vipo tayari kwa ajili ya kukabiliana na homa ya ebola.

Alisema hadi sasa jumla ya watumishi wanane wamepewa jukumu la kushughulikia homa ya ebola ambapo wanakagua watu wote wanaoingia nchini kupitia mpaka wa Tunduma.



HABARI DODOMA

# Waliopisha ujenzi wa SGR sasa walipwa fidia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limewalipa fidia ya kiasi cha Sh. bilioni 4.8 kwa wananchi 2,076 wa eneo la Ihumwa kutokana na maeneo yao kuchukuliwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Maeneo yao yalitwaliwa mwaka 2016 ili kupitisha reli hiyo.

Akizungumza wakati wa utoaji hundi, Meneja Msaidizi wa mradi wa SGR, Mhandisi Christopher Mang'wela, alisema fedha hizo zinatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 ambayo inasema endapo serikali itachukua ardhi kwa ajili ya manufaa ya umma lazima mwananchi alipwe fidia.

Alisema fidia ambazo wanapaswa kulipwa ni pamoja na eneo la makazi, mashamba, majengo na ardhi, lakini eneo la makaburi wahusika watapewa kifuta jasho na si fidia kama maeneo mengine.

"Tunawashukuru wananchi na kuwapongeza kutokana na kukubali kutoa maeneo ili ujenzi ufanyike maendeleo haya ni matokeo ya kila Mtanzania," alisema.

Alieleza kuwa utoaji hundi hizo utafanyika kwa wale ambao tayari wamehakikiwa na wapo kwenye orodha ya watu wanaopaswa kulipwa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, aliwataka wananchi wa eneo hilo kutumia fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na si kwenda kuongeza mke na kuleta migogoro ndani ya familia.

Alisema fedha walizopata ni nyingi lakini serikali kwa kuzingatia umuhimu wa wananchi imewasogezea Benki ya NMB, NBC kwa ajili ya wananchi wa eneo hilo kufunga akaunti kwa ajili ya kuhifadhi fedha hizo.

"Fedha hizo ni nyingi ila zisiwape kiburi cha kuzitumia ovyo na kuleta matatizo mtaani mkifanya hivyo rumande itawahusu," alisema Katambi.

"Wala msiwarubuni wanafunzi hela itawahusu zitumieni kuboresha miundombinu ya nyumba zenu," alisema.

Alisema awali serikali iliviomba vitongoji 57 vya eneo hilo kutoa ardhi kwa ajili ya maendeleo ya nchi, ambapo walikubali na sasa wanalipwa fidia.

Alisema Rais John Magufuli ameamua kutoa fedha hizo ili wananchi wa eneo hilo wasiwe maskini na kuwataka watu walipwe ili wawekeze kwa ajili ya maendeleo yao pamoja na jamii inayowazunguka.

Mmoja wa wananchi Christina Mganga, aliishukuru serikali kutokana na kuwajali kulipa fedha hizo ambazo wamezisubiri kwa muda mrefu.

Alisema serikali ya awamu ya tano imeonyesha jinsi gani inawajali wananchi wake kwa kuwalipa fidia hiyo ambayo wataenda kuendeleza shughuli za kilimo katika maeneo mengine.



Mchungaji Hamprey Sam (kushoto) wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Dodoma, Mtaa wa Kisasa, akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa watoto wa Shule ya Msingi ya wasioona Buigiri iliyopo Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, ikiwa ni mchango kutoka Jumuiya ya Bethsaida ya kanisa hilo, msaada huo ulikabidhiwa juzi shuleni hapo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali kukabiliana na uhaba wa malisho

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka wadau na wataalamu wa malisho kuboresha nyanda za malisho na maeneo ya machunga ili kuondokana na uhaba wa malisho.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angello Mwillawa, alipokuwa akifunga mafunzo rejea ya siku mbili yaliyowakutanisha wadau wa sekta hiyo.

Dk. Mwillawa alisisitiza lengo la uzalishaji huo ni kuwa na malisho yanayozaa kwa wingi na yana ubora unaomsaidia mnyama kupata virutubisho sahihi.

"Kuna wakati nchi iliwahi kukumbwa na ukame na idadi kubwa ya mifugo ilikufa sitamani kuona hali hii inajirudia tena wakati wataalamu wapo," alisisitiza Dk. Mwillawa.

Alisema wizara imekuwa ikitekeleza mkakati wa upatikanaji wa malisho na maji kwa nchi nzima ili kuhakikisha wafugaji wanapata tija.

"Tumekuwa tukihakikisha zile nyanda zetu za malisho wafugaji wanapata elimu ya kutosha na watumiaji wengine wa nyanda za malisho kwa kuhakikisha kunakuwa na matunzo na matumizi endelevu ya malisho," alisema.

Aidha, Dk. Mwillawa alisema kumekuwapo na mikakati mbalimbali ya wizara ikiwa ni pamoja na udhibiti wa magonjwa ya mifugo na matumizi ya dawa na viuatilifu kuhakikisha mifugo ipo katika ubora unaotakiwa.

Naye Ofisa Mifugo Mkuu Idara ya Malisho na Rasilimali za vyakula vya mifugo kutoka wizara hiyo, Israel Kilonzo, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwa na uelewa wa pamoja katika uzalishaji wa malisho na kutunza nyanda za malisho.

Mkuu wa Chuo cha LITA Mpwapwa, Moses Mlahagwa, alisema ili mifugo izalishe maziwa na nyama ya kutosha lazima wapate chakula cha kutosha.

"Hii imekuwa ni changamoto katika uzalishaji wa mazao ya mifugo yamekuwa ni hafifu kwa sababu hakuna lishe ya kutosha, hapa kwenye mafunzo tumeona changamoto hizi sasa tunaweza kuchukulia kama fursa ya kupiga hatua kwenye uzalishaji," alisema.

Hata hivyo, alisema chuo hiko kipo kwenye mpango wa kuwa na maeneo makubwa ya uzalishaji malisho hivyo ni fursa nzuri kwao kuhakikisha wanaingia kwenye eneo la uzalishaji kwa kupata uzoefu wa kutosha kutoka kwa wadau wengine.

Meneja Masoko kutoka Ranchi ya Taifa (Narco), Mzava Emmanuel, alisema kuna wakati nchi iliwahi kukumbwa na ukame na mifugo kufa haipaswi kujirudia tena kwa kuwa wataalamu wapo.

Ofisa Mifugo kutoka shamba la mifugo Mabuki na mtaalamu wa malisho, Asteria Mwaya, alisema ili kuwa na mbegu bora ya malisho kunapaswa shamba liandaliwe vyema, kuvunwa na kuhifadhiwa vizuri.

# Watoto kaya maskini kupata bima za afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATOTO 100 ambao wanaishi katika kaya maskini katika Jiji la Dodoma wanatarajiwa kadi za Bima ya Afya (NHIF) na taasisi ya inayojishughulisha na masuala ya watoto Sachia Society ili waweze kupata huduma za afya kwa urahisi.

Hayo yalielezwa jana na Mkurugenzi wa Utawala wa taasisi hiyo, Nsia Paul, wakati akitoa kadi hizo kwa watoto 33 wa mtaa wa sekondari kata ya Makutupora, jijini Dodoma.

Mkurugenzi huyo alisema taasisi hiyo inatoa huduma bure kwa watoto wenye umri wa kati ya miaka saba hadi 17 ambao ni yatima, wenye ulemavu, wanaoishi kaya maskini na wasichana waliokosa nafasi ya kujiendeleza kielimu.

Alisema watoto 100 watapatiwa kadi hizo kwa awamu ya kwanza katika mitaa nane ya jiji hilo.

"Wazo hili ni la Mkurugenzi wetu mkuu, Herieth Paul, ambaye alilipata alipokuwa akimalizia masomo yake ya elimu ya sekondari nchini Canada akiwa na umri wa miaka 17, aliona kufanya jambo la ziada kwa kuwasaidia watoto wenye umri mdogo," alisema.

Paul alisema lengo la taasisi hiyo ni kuhakikisha kwamba baadhi ya watoto wanapata nafasi ya kutimiza malengo yao waliyokusudia.

Alitoa wito kwa asasi nyingine za kiraia kujielekeza katika kusaidia watoto na vijana walio katika mazingira magumu ili waweze kutimiza ndoto zao na kushiriki kwenye harakati za kimaendeleo.

Akikabidhi kadi hizo, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, aliwataka wananchi kujiunga na bima ya afya kwa kuwa zinasaidia kurahisisha kupata matibabu pindi wanapokuwa na maradhi.

Alishukuru taasisi hiyo kwa kuwagusa watoto hao ambao watakuwa na uhakika wa afya zao kwa mwaka huu.

Alitoa rai kwa mashirika na wadau wengine kusaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.





# UWT waambiwa wabadilike

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

VIONGOZI na wanachama wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa Kaskazini Unguja, wametakiwa kubadilika kufanya maamuzi sahihi.

Uamuzi huo unatakiwa kuwachagua viongozi wenye uwezo na ari ya kuwatumikia na kukijenga chama na taifa.

Uamuzi huo wa kuwachagua viongozi bora na wenye uwezo utakisaidia Chama Cha Mapinduzi kuendelea kuongoza taifa.

Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Asha Suleiman Iddi, alieleza hayo wakati akilifungua kongamano maalum la umoja wa wanawake Tanzania Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema kupatikana kwa viongozi bora kunatokana na maamuzi wa wanachama wenyewe kupitia demokrasia ya chama kwa kuwapa fursa ya kuwachagua viongozi wanaowataka.

Alieleza kuwa kiongozi bora ni yule mwenye uwezo wa kuwaunganisha wanachama na kuwaletea maendeleo kwa wakati.

Aliwataka kinamama hao wa Mkoa wa Kaskazini kutumia muda wao kwa kuyatangaza yale yote mazuri yaliotekelezwa na serikali ya Chama Cha Mapinduzi kupitia viongozi hasa Rais John Magufuli na Dk. Shein wakiwa watekelezaji wakuu wa ilani ya uchaguzi waliyoinadi kupitia kampeni zao za mwaka 2015.

Mama Asha, alieleza kwamba kuelekea kwenye uchaguzi mkuu ipo haja kwa wanachama kudumisha utaratibu wa kujenga utamaduni wa kupendana, kuheshimiana na kudumisha mshikamano miongoni mwao.

Aidha, kuachana na tabia za majungu zinazoeneza sumu na chuki kwa kupeana sifa mbaya kila wakati.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Tunu Kondo, alisema lengo la kuadhimisha wiki ya umoja wa wanawake ni kuwakumbuka wazazi, wanachama na waasisi waliotangulia mbele ya haki ambao wametoa mchango mkubwa katika taifa hili.

Tunu alisema kuna kila sababu ya kuwakumbuka waasisi hao kwa vile walijitoa muhanga na kupigania uhuru wa kweli hasa wanawake kwa kupata fursa mbalimbali ikiwamo fursa ya kupiga kura, kushiriki katika vyombo vya maamuzi na kujitokeza hadharani kujinadi mambo ambayo hapo awali hakukuwa na fursa kama hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Thwaiba Edington Kisasi, aliwapongeza wanawake wa Mkoa wa Kaskazini kwa kuongoza katika kuibeba dhana ya kufanya makongamano kufuatia ngazi ya taifa kutekeleza suala hilo katika mikoa tofauti ya Tanzania.

Alisema kutokana na kujipanga ana imani kubwa ya kufanya vizuri kwa kukisaidia chama kuendelea kupata ushindi mnono kwenye uchaguzi ujao na wa mwaka 2020 na kuendelea kuifanya kaskazini kuwa ngome ya chama hicho.

Katika kongamamano hilo mada kadhaa ziliwasilishwa ikiwamo umuhimu wa daftari la kudumu la wapiga kura, kupinga vitendo vya udhalilishaji, umuhimu wa Jumuiya ndani ya chama na lishe bora.

# Walimu waahidiwa kuendelea kusoma

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, itaendelea kuwapatia mafunzo walimu kuimarisha taaluma za utendaji kazi.

Naibu Waziri, Simai Mohammed Said, alisema hayo na kuongeza kuwa ili walimu wafanye kazi kwa ufanisi ni lazima kuwaendeleza kielimu.

Said aliyasema hayo katika maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani, iliyofanyika katika uwanja wa Gombani Pemba.

Aidha, alisema serikali imejenga shule za kisasa zenye maabara za sayansi katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za elimu nchini.

Pia alisema wizara hiyo imewalipa walimu malimbikizo mbalimbali wakiwamo waliorudi masomoni.

Said alisema Wizara ya Elimu itaendelea kuangalia namna ya kuziboresha nafasi za walimu wakuu, kuwapatiwa ajira vijana waliosomea ualimu kadri hali itakavyoruhusu na kuwapa mazingira bora ya kazi.

Aidha, aliwataka walimu na umoja wa walimu Zanzibar kushirikiana ili kuleta maendeleo ya elimu na kuzalisha wataalamu waliobobea katika fani mbalimbali. Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrisa Muslim Hijja, alisema sherehe za Siku ya Walimu Duniani, zinasherehekewa na walimu wote.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman, aliwataka walimu kushirikiana na jamii kumaliza vitendo vya udhalilishaji hasa kwa watoto wadogo kwani ndiyo wanaodhalilishwa mno.



Ujenzi wa mradi wa machinjio ya Vingunguti ukiendelea ambapo mafundi wakiwa katika harakati za kuuwezesha kukamilika kwa wakati kulingana na mkataba. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Apongeza wananchi kushirikiana na SMZ

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI imeikabidhi kampuni ya Mecco kazi ya ujenzi wa barabara ya Fuoni Mambosasa hadi Mwera Melisita itakayojengwa kwa kiwango cha lami.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheir, ndiyo aliyeikabidhi Mecco jukumu hilo jana.

Aidha, Waziri Kheir aliwapongeza wananchi wa maeneo itakayopita barabara hiyo kwa kujitolea kuondoa vipando (mashamba) vyao nyumba kuridhia kufanyika ujenzi wa barabara hiyo.

"Nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wa maeneo haya kwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kuwapelekea karibu wananchi wake huduma za kijamii kwa kukubali kutoa maeneo yao na kutekelezwa kwa mradi huo," alisema.

Akizungumza huko Fuoni Mambosasa, baada ya kuikagua na kukabidhi, Kheir alisema ujenzi wa barabara hiyo ni utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ali Mohamed Shein, ya kuimarishaji barabara za ndani.

Alisema kumalizika kwa barabara hiyo ni kuimarisha mawasiliano ya usafiri wa barabara hus○sani kwa wananchi. Aidha, alieleza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, itaendelea kuimarisha miundombinu ya barabara za ndani katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar ili kuinua uchumi wa wananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mkuu wa Idara Maalum za SMZ katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa, Ali Omar Ali, alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 3.4 ya Fuoni Mabosasa hadi Mwera Melisita itagharimu Sh. bilioni 3.59 itajengwa kwa kiwango cha lami.

Alisema hakuna fidia itakayotolewa kufuatia ujenzi wa barabara hiyo na wananchi wameridhia utekelezaji wa mradi huo na kuwaomba watoe ushirikiano wakati wa ujenzi utakapoanza muda wowote kuanzia mwezi huu.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo pia utahusisha ujenzi wa daraja liliopo katika maeneo hayo pamoja na kuondosha njia ya umeme iliyopita eneo la ujenzi wa barabara hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya ujenzi ya Mecco, Abdulkadir Mohammed, alisema ujenzi huo utachukuwa miezi mitano na kumalizika Februari mwakani.

Ujenzi huo wa barabara ya Fuoni Mambosasa hadi Mwera Meli Sita yenye urefu wa kilo mita 3.4 unaojengwa na kampuni ya kizalendo ya Mecco unafanyika baada ya kampuni hiyo kumalizika daraja la Fuoni Kibonde Mzungu na barabara ya Kinuni.

# Walimu walia ukosefu wa ofisi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WALIMU wa Shule ya Sekondari ya Isakajana iliyoko Msalala mkoani Shinyanga, wamemlilia Mbunge wa Msalala (CCM), Ezekiel Maige, kuwa wanatumia maabara kama ofisi na kushindwa kuwafundisha wanafunzi masomo ya sayansi kwa vitendo na inapofikia wakati wa mitihani ya mwisho ya kitaifa wanalazimika kuhamisha ofisi chini ya miti.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Jana Likaya, aliyasema wakati Maige alipofanya ziara shuleni hapo. Katika ziara hiyo Mbunge huyo wa Msalala, Ezekiel Maige, aliwataka walimu wa Sekondari ya Isakajana iliyopo Msalala kuacha kujiingiza kwenye mambo ya siasa badala yake wafundishe wanafunzi. "Mheshimiwa Maige hivi karibuni tutakuwa na mitihani ya wanafunzi wetu wa kidato cha nne, na sisi tunatumia maabara kama ofisi ya mwalimu mkuu na walimu wote. Itatupasa tuhamishe ofisi yetu chini ya miti na mvua itakaponyesha itatulazimu kutumia moja ya darasa," alisema Likaya.

Mwalimu mwingine, Simba Mlamba alimwambia Maige kuwa, mwaka jana shule ilifanya vema kwenye mitihani ya kitaifa na kushika nafasi ya kwanza katika Halmashauri ya Msalala na nafasi ya tatu kimkoa, na kuwataka walimu wenzake kuendelea kuwafundisha wanafunzi ili waendelee kufanya vema kila mwaka.

Akijibu hoja ya kujihusisha na siasa Mwalimu Mkuu, aliahidi kuwa kama kuna mwalimu atabainika kujihusisha na masuala ya kisiasa wakati wa masomo hatasita kumchukulia hatua za kinidhani na kuwataka walimu kuendelea kufundisha na kuwaleta wanafunzi katika maadili mema.

Maige ambaye jana alikuwa akizungumza na walimu wa shule hiyo alidai kuwa shule nyingi nchini, wanafunzi wake washindwa kufanya vema katika mitihani yao ya mwisho kutokana na walimu kutumia muda mwingi kwenye siasa.

Aliwaambia kuwa wamekuwa wakitumia muda mwingi kwenye kujadili masuala ya siasa badala ya kufundisha na kusababisha wanafunzi kukosa masomo kwa muda mrefu kuifanya halmashauri kufanya vibaya katika mitihani ya kitaifa.

"Kwa sasa tunatumia muda mwingi kwenye kujadili masuala ya kisiasa badala ya kuwafundisha na hili suala limekuwa likisababisha wanafunzi kushindwa kufanya vema kwenye mitihani yao ya mwisho kutokana na kukosa masomo," alionya Maige

# Washangilia ujio wa maji shuleni

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANAFUNZI wa Sekondari ya Hawa Mchopa ya wilayani Ruangwa Mkoa wa Lindi, wanaishukuru serikali kuwasogezea huduma ya majisafi na salama na kuwaondolea tatizo la kufuata huduma hiyo umbali mrefu.

Shukrani hizo wamezitoa jana walipokuwa wanazungumza na wanahabari waliotembelea shuleni hapo kuona kazi za maendeleo.

Wanafunzi Abdallah Daudi, Michael John, Mwanajuma Isumaili, Amina Selemani wa kidato cha pili, tatu na nne wakizungumzia kwa niaba ya wenzao, walisema tangu huduma hiyo ipatikane shuleni hapo, kumesaidia kuboresha afya zao na mazingira ya shule yao.

"Hivi sasa tumekuwa na uhakika wa kunywa majisafi na salama, tunaoga na kufua bila shida, tunaipongeza serikali ya awamu ya tano," alieleza mwanafunzi Mwanajuma.

Pia walieleza kwamba kabla ya huduma hiyo, walilazimika kutembea zaidi ya kilomita tatu kufuata maji vijiji jirani kabla ya kuanza masomo kila wakati ili wapate ya kunywa, kufulia nguo, kuoga na kupigia deki vyumba vya madarasa ya shule yao.

Aidha, walitaja changamoto nyingine walizokuwa wanazipata kabla ya mradi huo kuwa ni pamoja na msongamano wa watu visimani, upatikanaji wa maji kwa mashaka, kwani walikuwa wakikaa muda mrefu bila ya kuwa na uhakika wa kupata.

Hamisi Kabera ni mwalimu shuleni hapo, anasema Hawa Mchopa Sekondari, kuwapo maji kumewezesha kuwajenga wanafunzi kiakili kuamini shule na kuwaimarisha kimawazo kuelekeza kwenye zaidi katika masomo badala ya kufikiria wapi wataweza kupata huduma hiyo ambayo ni muhimu kwa viumbe karibu wote.

Mwalimu Kabera alisema kwa kutambua changamoto hiyo, serikali imepeleka shuleni hapo miradi miwili ya maji, ukiwamo wa bomba na kisima cha kata, hivyo kuondoa kwa kiwango kikubwa tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo.

"Tunaishukuru serikali imetuondoa kwenye tatizo la upatikanaji wa maji na sasa tuna uhakika wa upatikanaji wa huduma hii," alisema Kabera.

Shule ya Sekondari Hawa Mchopa iliyoanzishwa mwaka 2008, ina wanafunzi 442, kati yao wasichana ni 245 na wavulana 197 huku ikiwa na walimu 12, wanawake ni wawili.



Mhandisi kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Elisante Ulomi, akimwonyesha maendeleo ya ujenzi wa mradi wa Machinjio ya Vingunguti Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa mradi huo jana. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

# 'Ardhi ikisajiliwa huondoa migogoro'

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Pemba Omar Khamis Othman, amewataka wananchi kusajili ardhi wanazomiliki ili kuondosha migogoro isiyo ya lazima.

Alisema kuwa usajili wa ardhi ni jambo muhimu, hivyo wananchi wasipuuze wachangamke kwani manufaa yapo ya sasa na ya baadaye.

Mkuu huyo aliyasema hayo wakati akizungumza na viongozi mbali mbali wa wilaya hiyo wakati wa ufunguzi wa semina ya usajili wa ardhi na mirathi iliyoandaliwa na Kamisheni ya Ardhi.

Othman alifahamisha kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mamlaka za kusimamia ardhi imeanzisha utaratibu wa kusajili ardhi kwa lengo la kupunguza migogoro miongoni mwa wananchi.

"Migogoro mingi ya ardhi inatokea katika jamii kutokana na wananchi wengi kutokuwa na utamaduni wa kuzirasimisha ardhi zao katika mamkala husika," alisema Omar.

Aidha, Othman alizitaja faida ambazo zinapatikana katika kusajili ardhi kuwa ni pamoja na kupata mikopo katika taasisi za fedha, kumtambua mmiliki kwa urahisi pamoja na kujua ardhi ilipo, ukubwa wake na matumizi yake.

Akizungumzia suala la mirathi Mkuu wa Mkoa alisema kwa sasa limekuwa ni tatizo kubwa ndani ya jamii, hivyo inapaswa kupewa kipaumbele na jamii kuhamasishwa kuhusu umuhimu wa kufuata sheria na taratibu.

"Mirathi si jambo la kulifanyia mzaha kwani ni haki za watu ambazo hatuna budi kuzichunga, kuzilinda na kuwapatia sambamba na kuzingatia wosia wa marehemu," alisema.

Mkuu wa Mkoa aliwataka viongozi hao kutumia nafasi walizonazo katika jamii ili kufahamisha faida na hasara za kutokusajili ardhi na kutenda haki ya mirathi.

Akifunga semina hiyo, Katibu Tawala Wilaya ya Wete, Mkufu Faki Ali, alisema kuwa migogoro ya ardhi imekuwa ni changamoto kubwa katika jamii kwani kila siku wamekuwa wakipata malalamiko juu ya masuala hayo.

Aliipongeza Kamisheni ya Ardhi kutokana na uamuzi huo wa kuzungumzia ardhi, akisema kuwa wamepata mwamko wa kuweza kupambana na changamoto za matatizo hayo.

"Lakini niwashauri wajumbe wote waliopatiwa nafunzo haya kuyachukua na kuyafanyia kazi, lakini pia tuwe walimu wazuri katika jamii yetu inayotuzunguka," alisema.

Aliwaomba wananchi kujitahidi sana na kujiepusha na migogoro ya ardhi na endapo itatokezea wakimbilie katika vyombo vya sheria ili kupata suluhisho.

Sheha wa Shehia ya Limbani, Massoud Ali Hassan, alieleza kuwa katika shehia yake wananchi wengi wamepata mwamko wa kusajili ardhi zao kwani ni miongoni mwa maeneo yasiyopimwa.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kushirikiana na serikali yao ili kupunguza migogoro ya ardhi.

Naibu Mkurugenzi wa Kilimo na Mazingira Wilaya ya Wete, Makame Hamad Said, alisema kuwa kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi ambayo haina maslahi kutokana na kugombania ardhi.

"Endapo tutasajili ardhi zetu tutaweza kupunguza migogoro ya ambayo kwetu haina maslahi kubwa ni kuwekeana chuki na uhasama katika jamii zetu," alisema Makame.

Katika mafunzo hayo mada mbalimbali ziliwasilishwa kuhusu mirathi na ardhi.

## HABARI KIMATAIFA

# Uchaguzi wa bunge wafanyika Tunisia

**TUNIS,** Tunisia

RAIA wa Tunisia wameanza kupiga kura kulichagua bunge jipya katika kipindi kigumu cha kisiasa ambacho chama cha siasa za wastani zinazoegemea Uislamu kikitarajia ushindi.

Aidha, vuguvugu la mfanyabiashara tajiri anayezuiliwa jela chama chake nacho kinatarajia kupata ushindi.

Katika uchaguzi huo itakuwa vigumu kwa chama kimoja kupata wingi wa viti, ingawa chama cha Ennahdha na kile cha tajiri aliye gerezani Nabil Karoui, vinatarajiwa kujikingia wingi wa kura.

Ulinzi umeimarishwa huku kiasi polisi na wanajeshi 100,000 wametawanywa kushika doria kwenye vituo 45,000 vya kupigia kura, zaidi katika mpaka kati ya nchi hiyo na Algeria pamoja na Libya.

Wasiwasi kuhusu hali ya uchumi ndiyo kipaumbele cha wapigakura ambao watachagua wabunge 217 kutoka orodha ya maelfu ya wagombea wanaowania kuingia bungeni.

Matokeo ya uchaguzi huo yanatarajiwa kutolewa Alhamisi inayokuja.

Wiki iliyopita wafuasi wa Karoui walisema kuwa hawatakubali kufanyika kwa uchaguzi huo ikiwa mmoja wa wagombea hao wawili atakuwa bado anazuiliwa jela.

Kufungwa kwa Nabil Karoui kumezua sintofahamu kwa uchaguzi wa urais ambao umepangwa kufanyika mwishoni mwa wiki hii.

Wajumbe kadhaa wa kamati kuu ya kisiasa ya chama chake cha Qalb Tounes, walikutana Jumatano iliyopita.

Waliitilia mashaka duru ya pili ya uchaguzi wa urais ikiwa kiongozi wao atakuwa bado anazuiliwa jela ndani.

Waliomba Tume Huru ya Uchaguzi (ISIE) kutafuta suluhisho haraka. "Ni juu yao kutafutia suluhu hali ambayo si ya kawaida inayomkabili mgombea wetu aliyechaguliwa akiwa jela. Wanapaswa kupata ufumbuzi, sio sisi, " Osama Khlifi, mjumbe wa kamati kuu ya kisiasa ya chama cha Qalb Tounes, alisema.

Mwenyekiti wa ISIE aliomba mara kadhaa Nabil Karoui kuachiliwa huru ili kuhakikisha usawa kuwania na fursa kwa wagombea wote wawili. **DW**



Raia wa Tunisia akipita pembeni ya ukuta wenye matangazo ya baadhi ya wagombea katika uchaguzi. **PICHA: MTANDAO**

# IMF kurudisha misaada DRC?

**KINSHASA,** Congo

SERIKALI ya Kinshasa, inasema Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), linafikiria kuidhinisha upya ushirikiano wa kifedha na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo katika miezi sita ijayo, shirika la habari la Reuters imeripoti.

Awali IMF lilisitisha msaada wa kifedha wa Serikali ya Congo, miaka takriban saba iliyopita chini ya utawala wa Joseph Kabila baada ya serikali hiyo kushindwa kutoa taarifa za kutosha kuhusu mauzo ya madini kwa kampuni za kigeni.

Katika taarifa kufuatia kikao cha Baraza la Mawaziri, serikali ilisema: "IMF litakagua katika muda wa miezi sita mpango wa muda mfupi na serikali," taarifa hiyo haikutoa maelezo zaidi, kwa mujibu wa vyombo vya habari.

Shirika hilo linafikiria ushirikiano mpya wa kifedha na Congo kufuatia majadiliano mapya kati ya pande hizo mbili, Reuters, ilisema ikimnukuu Waziri Mkuu wa Congo Sylvestre Ilunga.

**Congo ni mchimbaji wa madini ya cobalt, shaba, dhahabu, tin na almasi lakini taifa hilo linasalia kuwa mojawapo ya mataifa yanayoshuhudia maendeleo duni mno duniani.**



Rais wa Congo, Felix Tshisekedi (kushoto) na mstaafu Joseph Kabila, katika moja ya mikutano ya kisiasa kujadili mambo ya uongozi. **PICHA: MTANDAO**

Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo imebarikiwa kuwa na madini mengi pamoja na maliasili lakini zimeathiriwa na vita vinavyosababishwa na vikundi vya waasi, rushwa, machafuko ya kisiasa na hivi sasa tatizo la ugonjwa wa ebola.

Congo ni mchimbaji wa madini ya cobalt, shaba, dhahabu, tin na almasi lakini taifa hilo linasalia kuwa mojawapo ya mataifa yanayoshuhudia maendeleo duni mno duniani. **BBC**



Mmoja wa waandamanaji akichoma matairi mitaani. **PICHA: REUTERS**

# UN yakemea mauaji nchini Iraq

**NEWYORK,** Marekani

UMOJA wa Mataifa (UN) umetaka 'mauaji ya watu yasio na maana' yasitishwe nchini Iraq mara moja.

Wakati inatoa maagizo hayo, idadi ya raia waliouawa kutokana na maandamano ya kuipinga serikali inakaribia 100.

Waandamanaji walisema wanachukua msimamo dhidi ya ukosefu wa ajira, huduma mbovu za umma na ufisadi nchini humo. Jeanine Hennis-Plasschaert, Mkuu wa Kitengo cha Ujumbe wa Msaada kwa Iraq -UN alisema: "Siku tano za mauaji na majeruhi: ni lazima lisitishwe."

Waliohusika na vifo vya watu wanapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria, alisema.

Juzi Jumamosi, vikosi vya usalama vilitawanya maandamano ya umma mashariki mwa Baghdad.

Watu watano wanaarifiwa kufariki katika mapigano ya hivi karibuni katika mji huo mkuu na vikosi vya usalama vinaripotiwa kwa mara nyingine kutumia risasi za moto na gesi ya kutoa machozi.

Takriban watu 99 wamefariki na wengine karibu 4,000 wamejeruhiwa tangu kuanza kwa ghasia katika mji mkuu huo Jumanne kabla ya kusambaa kusini mwa Iraq, kwa mujibu wa Tume ya Haki za Binadamu ya Bunge la Iraq.

Ni ghasia mbaya kuwahi kushuhudiwa tangu kutangazwa, kushindwa kwa kundi la Islamic State nchini humo mnamo 2017.

Ilionekana kama changamoto ya hivi karibuni kwa serikali dhaifu ya Waziri Mkuu Adel Abdel Mahdi, takriban mwaka mmoja tangu aingie madarakani. Maofisa wa utawala wake wamekuwa wakijaribu kudhibiti maandamano hayo kupitia kuidhinishwa marufuku ya kutoka nje na kuzimwa kwa mtandao nchini.

Marufuku iliyoidhinishwa mchana ya kutoka nje Baghdad iliondolewa Jumamosi na makundi madogo ya waandamanaji wakaanza kukusanyika tena.

Midani ya Tahrir ndiyo sehemu ambapo waandamanaji wanamiminika lakini ilifungwa Jumamosi kwa mujibu wa mashirika ya habari nchini.

Kikao cha dharura cha bunge kilishindwa kuendelea juzi Jumamosi mchana.

Vituo kadhaa vya televisheni vilishambuliwa zikiwamo ofisi za kituo cha habari kinachomilikiwa Saudia - Al-Arabiya.

Huko Nasiriyah, waandamanaji waliteketeza moto makao makuu ya vyama sita tofauti vya kisiasa. **BBC**

# Magufuli awaweka pagumu

INAENDELEA UK. 2

**TAASISI/MASHIRIKA SIKU 30**

Aidha, Rais Magufuli alitoa mwezi mmoja kwa taasisi au mashirika ya umma kuhama kwenye majengo binafsi na kuhamia kwenye ofisi za serikali zilizoachwa wazi.

"Hili ndilo tatizo kuwa kwa taasisi kupanga kwenye nyumba pamoja na kwamba majengo ya serikali yapo na kwamba Dar es Salaam serikali zimehama lakini bado wamepanga," alisema.

**AAGIZA MKANDARASI KUBANWA**

Alisema mkataba na mkandarasi wa mradi wa maji wa eneo hilo ni wananchi wapate maji naye apate fedha, lakini imekuwa kinyume chake kwa kuwa amepata pesa Sh. bilioni 7.1 na maji hakuna huku sola zaidi ya 150 zimechomwa moto.

Aidha, alihoji kama wahusika wamekamatwa na kufikishwa mahakamani, huku akiwaita viongozi mbalimbali kueleza hatua zilizofikiwa na kuagiza wafikishwe mahakamani. Rais Magufuli alisema kuna miradi ya Sh. bilioni 20, Nkasi, Kalambo mkandarasi ni huyo huyo, bado aliendelea kupewa zabuni nyingine za kutekeleza miradi ambayo haikamiliki.

Aidha, alimhoji Mkuu wa Takukuru, ambaye alieleza kuwa tukio lina miezi miwili na kwamba wanachukuza hadi Novemba watafikishwa mahakamani.

Rais hakuridhishwa na maelezo ya kiongozi huyo kwa kuwa wanachunguza muda mrefu, huku akimuita Kamanda wa Polisi wa mkoa, ambaye alisema uchunguzi umekamilika na watu wawili wanashikiliwa na wameshapeleka jalada kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa ajili ya hatua zaidi.

"Walikamatwa wawili na wapo nje kwa dhamana," alisema RPC na Rais kuhoji, kwanini wapo nje kwa dhamana, Sh. bilioni saba zimepotea, Waziri anatoa maelekezo hayasikilizwi, waziri nimemteua mimi halafu bado uitwe RPC," alisema.

Rais Magufuli aliagiza RPC kutuma maagizo muda huo huo ili wahusika wakamatwe huku akitoa siku saba Takukuru na RPC na wengine wanaohusika wapelekwe mahakamani, miezi miwili unapeleleza mambo ya ajabu sana, nitafuatilia mwenyewe," alisema.

Aidha, alimwagiza Waziri wa Maji kufuatilia waliokuwa wanaotoa zabuni kwa mtu huyo huyo, pia watu wa manunuzi na mkandarasi wa miradi hiyo.

"Miradi yote ifanyiwe tathmini upya na kwamba wataondoka na watu, Mheshimiwa Ally Kessy amelalamika sana watu wanampuuza, niwaeleze viongozi wenzangu sina mchezo," alisema.

Rais alimkaribisha Mbunge wa Nkasi, Kessy ambaye alieleza kuwa mkandarasi huyo amepewa miradi lakini hakuna hata mmoja unaokamilika na kwamba amejenga ghorofa kwa miradi ya maji na kwamba atapike hizo pesa, haiwezekani wananchi wanakufa kwa kipindupindu.

Rais alisema: "Mheshimiwa Waziri nataka ufanye uchunguzi timu yako ije huku au ikiwezekana ubaki huku huku, nimekaa Wizara ya Ujenzi miaka 17 najua, viongozi wafuatilie akiwamo mkurugenzi," alisema.

**ASKARI TISA WAFUKUZWE**

Rais Magufuli aliagiza kutekelezwa kwa agiza la Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, la kuondoa askari tisa wa kituo cha Laela wanaodaiwa kuhusika kubambikia kesi na kuwanyima dhamana kwa makosa ambayo yana dhamana.

Rais alimwita RPC na kumuuliza utekelezaji wa jambo hilo na ikaonekana halijatekelezwa kwa kuwa RPC hakupata maelezo kutoka kwa aliyekuwa amemwachia ofisi.

"Watu mna dharau sana eehh, unafikiri nikitamka utaendelea kuwa RPC, kwanini Waziri wenu wa Mambo ya Ndani ametoa maelekezo halafu hayafuatwi, sasa katekeleze maagizo haya kabla sijafika Sumbawanga, nikifika huko nipate majibu, msipotekeleza nitatekeleza yangu mimi kwako na kwa OCD uliyemwachia," alisisitiza

**AAGIZA POLISI ASIMAMISHWE**

Rais alimpigia Mkuu wa Polisi Nchini, IGP Simon Sirro, kumsimamisha kazi ofisa wa Jeshi la Polisi Rukwa, Polycarp Urio, hadi atakapotoa maelekezo mengine.

Alitembelea kituo cha polisi Laela na kumuuliza RPC kwanini hakutekeleza agizo la waziri, alijibu hakujua kwanini hakutekeleza licha ya kupewa majina.

"Nataka apewe amri na nani, aliambiwa awahamishe? Amri ya kuhamisha halafu hatekelezi, anafikiri huyo (Waziri) sikumteua, anaweza kutoa amri ya uongo lakini kazi ya jeshi ni kutii amri," alisema Rais.

Aidha, alitoa simu na kumpigia IGP na kumweleza RPC huyo kuwa alitaka amfukuze kwa kuwa hajatekeleza agizo hilo.

Akiwa kituoni humo alimpigia simu IGP na baada ya kupokea; "kuna Staff Officer wa polisi msimamishe kazi hadi nitakapotoa maelekezo," alisema.

**LUGOLA ANENA**

Waziri Lugola akihojiwa aliwataka watendaji wa vyombo vya dola kutambua mamlaka na kuheshimu na kwamba ameteuliwa na Rais na anapotoa maelekezo yanatakiwa kutekelezwa.

"Rais atafanya mambo mangapi, tunatoa maagizo lazima yafuatwe...tutaendelea kusimamia kwa sababu tumepewa mamlaka, tutaendelea kutoa maagizo na kwamba wanaofanya kutokutekeleza ni wachache sana na hatutawavumilia kabisa," alisema.



Meneja Uhusiano Msaidizi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), akizungumza na baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Benjamin William Mkapa kuhusu elimu ya fedha, ujasiriamali na stadi za maisha wakati yeye na wafanyakazi wenzake walipotembelea shule hiyo na kutoa elimu ikiwa ni sehemu ya majukumu ya kujitolea katika kuisaidia jamii. Hafla hiyo ilifanyika shuleni hapo, Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Sababu madaktari kupewa elimu mionzi

INAENDELEA UK. 5

teknolojia hii kwamba itawasababishia madhara," alisema.

Alisema wanapozungumzia teknolojia hiyo wamekuwa wakipata hofu, lakini nyuklia haina madhara kwa watumiaji.

Alisema Aga Khan kwa kushirikiana na kampuni ya Siemens waliamua kuwekeza katika teknolojia hiyo ya mionzi ya nyuklia hospitalini hapo miaka mitano iliyopita na hadi sasa zaidi ya wagonjwa 800 wamefanyiwa uchunguzi wa magonjwa mbalimbali yakiwamo tezi dume, moyo na figo.

Dk. Jusabani, alisema kati ya wagonjwa hao, asilimia 99 ni magonjwa kama moyo na figo.

"Huduma ya vipimo vya mionzi ya nyuklia inayotolewa na mashine hii ni bora na salama katika ugunduzi wa magonjwa. Inagundua magonjwa mwili nzima ya saratani na yasiyokuwa ya saratani na inapima wagonjwa wa umri wote kuanzia watoto wachanga wanaozaliwa hadi wazee," alisema.

Aliongeza kuwa Idara ya Radiolojia hospitalini hapo imekuwa mwanzilishi wa teknolojia nyingi ikiwamo ya MRI iliyoanza kutolewa 2010.

Alisema changamoto ni kwamba katika utumiaji wa teknolojia hiyo lazima wapate vitendea kazi ambavyo hutoka nje ya nchi na visipofika kwa wakati, haviwezi kutumika.

Naye Meneja wa Masoko na Mawasiliano hospitalini hapo, Olayce Lotha, alisema mashine hiyo ikilinganishwa na nyingine ni ya kisasa na mionzi yake ipo chini.

## AAR yakutanisha kampuni 20 kufanya mazoezi, kupima afya

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya Bima ya AAR inayotoa bima ya afya na bima za jumla, imewakutanisha wafanyakazi wa kampuni zaidi ya 20 jijini Dar es Salaam kushiriki katika michezo mbalimbali na kupima afya zao bure.

Akizungumza na waandishi wa habari katika tukio hilo lililofanyika mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya Posta, Kijitonyama jijini, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Violet Modichai, alisema wameamua kuwakutanisha wadau wao na kushiriki nao katika michezo kama njia ya kuwahamasisha kuepuka magonjwa yasiyoambukiza ambayo hugharimu uchumi wa nchi na uchumi wa mwananchi mmojammoja.

"Hatua hii ni kuunga mkono juhudi za serikali yetu ambayo imekuwa ikihamasisha wananchi kushiriki katika mazoezi ili kuondokana na magonjwa yasiyoambukiza ambayo hugharimu uchumi wa nchi na kufifisha nguvu kazi ya Taifa," alisema Modichai.

"Magonjwa hayo ambayo yanatajwa kuwa mengi na kuwa chanzo cha vifo vingi nchini, yanaweza kuepukika kwa watu kushiriki katika mazoezi na kubadili mtindo wa maisha yao ikiwa ni pamoja na vyakula wanavyokula," aliongeza.

Alieleza kuwa nchi inapaswa kutengeneza mabalozi wengi zaidi wa kuhamasisha watu kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi pamoja na kupima ili kufahamu afya zao.

"Katika mabanda yetu tumewaleta madaktari wabobezi kwa lengo la kusaidia kutoa huduma za kupima afya bure, kwa maana ya kupima presha, kupima kisukari na pia kutoa elimu kuhusu milo ili kujenga jamii yenye afya bora," alisema Modichai.

## Bonite Bottlers yazindua promosheni

INAENDELEA UK. 4

kuisha Novemba 30.

Shindano hilo litahusisha maji ya Kilimanjaro ya ujazo wa nusu lita, lita moja na lita moja na nusu, droo kubwa mbili zitachezeshwa ambapo droo ya kwanza itakuwa mwanzoni mwa Novemba na droo ya pili itakuwa mwanzoni mwa Desemba ambapo mteja atatakiwa kununua angalau katoni kumi za maji ya Kilimanjaro ya ujazo wowote na kupewa tiketi ya kuingia katika shindano.

Zawadi kwa washiriki ambao watanunua kuanzia katoni mia mbili kwa mwezi watazawadiwa katoni za maji ya Kilimanjaro za ujazo wa nusu lita kuanzia katoni kumi na kuendelea, huku wengine wakijishindia bodaboda na televisheni ya ukubwa wa nchi 32.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: 0713 525954 / 0787 822000.

**VIWANJA/NYUMBA.** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Nyumba inauzwa Kaloleni Arusha ina frame za biashara,nyenye SQ 59 mil 800. Nyumba inauzwa Usariver ya bedroom4 mil 70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

## KUPOTEA KWA CHETI



115447602

**ANITHA CHARLES LUGEIYAMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0268-0001** kilichotolewa na BETHEL SABS GIRLS SEKONDARI November, 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. **9910810166864.**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0767 223311**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# SOLSKJAER AWAWEKA KWENYE RADA MANDZUKIC, WILSON

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amewaweka kwenye orodha ya kutaka kuwasajili, Callum Wilson wa Bournemouth na Mario Mandzukic wa klabu ya Juventus.

Solskjaer anamsaka washambuliaji wa kukitia nguvu kikosi chake kinacholegalega baada ya kuwaondoa Romelu Lukaku na Alexis Sanchez bila ya kuongeza mshambuliaji kikosini hapo.

Wachambuzi na mashabiki wa United wamekuwa wakimkosoa mshambuliaji, Marcus Rashford pamoja na makinda wengine katika safu ya ushambuliaji hawana uwezo wa kukibeba kikosi hicho katika safu ya ushambuliaji.

Juzi usiku United ilicheza mchezo wa Europa League dhidi ya AZ Alkmaar na haikufanikiwa kupiga shuti hata moja lililolenga bao katika mchezo huo uliomalizika kwa sare ya bao 1-1. Sasa Ole ni kama ameona tatizo hilo la washambuliaji na kuwafungia kazi mastaa hao.

# Bayern kumzuia Lucas kuichezea Ufaransa

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich haitamruhusu Lucas Hernandez kujiunga na kikosi cha timu ya Taifa ya Ufaransa kwa mechi za kimataifa, Mkurugenzi wa soka wa miamba hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Hasan Salihamidzic amebainisha.

Lucas alijumuishwa kwenye kikosi cha Ufaransa cha wachezaji 23 Ijumaa kilichotajwa na kocha, Didier Deschamps kwa ajili ya mchezo wa kufuzu kwa fainali za Euro 2020 dhidi ya Iceland na Uturuki.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alikosa mechi za mwisho mbili za Bayern akiwa ameumia goti na Salihamidzic amekataa kumruhusu kujiunga na timu ya taifa wakati akijiuguza.

Hivyo hivyo, kwa mchezaji wa kimataifa wa Austria, David Alaba, ambaye aliumia mbavu wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 7-2 kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Tottenham Jumanne.

"Tutazijulisha timu za taifa kwamba wachezaji bado hawapo fiti, wameumia. Halafu madaktari watazungumza," alisema.

Mabingwa hao wa Ujerumani wapo hatarini kuvunja kanuni za Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), lakini Salihamidzic aliongeza kwamba wachezaji wote wawili hawataondoka Bayern.







# Tuchel: Uhusiano wa Neymar, mashabiki PSG umeimarika

**PARIS,** Ufaransa

UHUSIANO kati ya nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar na mashabiki wa klabu "yamekuwa bora zaidi", kwa mujibu wa kocha Thomas Tuchel.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, Neymar aliifungia timu yake bao la nne wakati kikosi hicho kikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Angers kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, uliopigwa katika Uwanja wa Parc des Princes, juzi Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ana mabao manne kwenye mechi tano alizocheza msimu huu, na hiyo ni baada ya kufungwa kwa dirisha la usajili na kujikuta akibakia klabuni hapo.

Neymar alikuwa akitaka kurudi kwenye klabu yake ya zamani ya Barcelona, ingawa uhamisho huo ulishindikana, na alikuwa akizomewa na mashabiki kwa kitendo chake hicho.

Lakini sasa kocha Tuchel anafikiri kwamba mambo yameanza kubadilika na uhusiano kati yao unazidi kuimarika.

"Kuhusu Neymar, ndio, uhusiano unakuwa bora zaidi na rahisi," alisema wakati alipoulizwa kama kuna maendeleo yoyote kwenye uhusiano wao.

"Nilisema ni juu yetu, ni juu yake pia kuonyesha tena uwezo wake na kuwa mwamuzi wa mechi. Si muhimu zaidi kuzungumza.

"Ameonyesha mambo mengi, kwa kucheza vizuri na kuwa msaada kwa timu na alicheza kwa ubora zaidi kwenye mchezo dhidi ya Angers.

"Alifunga tena, na anaweza kufunga mabao zaidi, bado ana uwezo wa kufanya vitu vizuri zaidi."

HABARI MICHEZO

## Pochettino: Sina hofu kufukuzwa Tottenham

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino, amesema hahofii kufukuzwa licha ya kikosi chake kuwa na matokeo mabaya.

Spurs walifungwa mabao 3-0 na Brighton Jumamosi wakiwa wametoka kufumuliwa mabao 7-2 na Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Klabu hiyo pia ilitolewa kwenye Kombe la Carabao kwa mikwaju ya penalti na timu ya daraja la pili, Colchester, mwezi uliopita.

Wakati alipoulizwa kama anahofia kazi yake, Pochettino alisema: "Hapana, sihofia, ninachohofia mimi ni maisha, si soka."

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mchezo wa Jumamosi pale katika dimba la Amex, Pochettino alisema: "Soka ni mchezo ambao wakati mwingine unashinda, wakati mwingine unapoteza.

"Matatizo kwetu ni kushinda, kushinda, kushinda na kila moja alikuwa anasifia.

"Sasa katika mechi mbili zilizopita hali ilikuwa ni ngumu kuikubali. Lakini sitaki kuwa mwanafalsafa au kuongeza katika njia ambayo siyo nzuri."





## HAZARD ANATAKA MABAO ZAIDI REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard alishukuru kufunga bao lake la kwanza kwa Real Madrid Jumamosi wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Granada kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Hazard alifunga bao lake la kwanza tangu ametua hapo Madrid kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 100 akitokea Chelsea Juni mwaka huu na pia alitoa pasi ya mwisho kwa kikosi hicho cha kocha, Zinedine Zidane ambacho kimepanda kileleni mwa msimamo kwa pointi nne zaidi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alifurahia kuwa kwenye orodha ya wafungaji na sasa anatumaini kwamba mabao zaidi yatakuja kwa miamba hao wa La Liga.

"Nimefurahia kushinda, wakati unapocheza unataka kufunga, lakini jambo la muhimu zaidi ilikuwa ni ushindi. Bado tupo kileleni mwa msimamo wa ligi, hayo ndio malengo yetu," alisema Hazard akiiambia televisheni ya Real Madrid.

"Ilikuwa ni ngumu kupata bao la kwanza, lakini wakati ukilipata, unajiamini zaidi kupiga mashuti langoni na natumaini kufunga mabao mengi zaidi kwa klabu hii kubwa. Ilikuwa ni muhimu kwangu mimi kufunga.

"Hakika ilikuwa ni ngumu kupigania ushindi kwa sababu Granada walicheza vizuri, wana kikosi imara na ndio maana wapo nafasi ya pili kwenye msimamo wa La Liga, lakini tulijitoa kwa nguvu zote katika dakika zote 90 za mchezo ule."

## Ushindi Milan washusha presha kwa Giampaolo

**MILAN,** Italia

MARCO Giampaolo amemsifia golikipa Pepe Reina kwa kuokoa penalti ya dakika za majeruhi ya Genoa wakati AC Milan ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1, Juzi Jumamosi.

Kocha huyo wa zamani wa Sampdoria, Giampaolo alipata ushindi huo na kuendelea kujiweka kwenye nafasi kubwa ya kukinusuru kibarua chake, huku penalti ya Franck Kessie ndio ikiwapa ushindi huo muhimu.

Golikipa Reina, ambaye aliingia kuchukua nafasi ya Gianluigi Donnarumma, alicheza vizuri kuokoa penalti ya Lasse Schone, awali akiwa amemzawadia bao kiungo huyo wa Genoa kwa makosa ya kushindwa kuutoa mpira wa adhabu ndogo.

Ushindi huo umepunguza presha kwa Giampaolo, ambaye alipoteza mechi tatu kabla ya kuingia kwenye dimba hilo la Luigi Ferraris.

"Nilitulia kwa kipindi chote cha mchezo, bahati nzuri tulishinda," alisema Giampaolo akiiambia DAZN.

"Nilikuwa na shaka na penalti, lakini Reina alionyesha uwezo wake na nilikuwa na imani kubwa kwamba angeokoa.

"Ilikuwa mechi ngumu, tulikuwa kwenye presha kubwa, hivyo nashukuru kwa kile tulichokipata, maana pointi tatu zilikuwa muhimu zaidi kwetu."



Mkurugenzi wa Kampuni ya Bima ya AAR, Violet Mordichai, akikabidhi kombe kwa washindi wa mpira wa miguu, timu ya Southern Sun wakati wa Bonanza lililoandaliwa na AAR na kufanyika katika viwanja vya Posta, Kijitonyama Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VALVERDE AFUNGUKA SIRI MESSI, SUAREZ

## ●●● Tungependa wachezaji wakazichezee nchi zao kwenye mechi za kimataifa, lakini tu kama...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi na Luis Suarez wako fiti kwa Barcelona, lakini Ernesto Valverde malengo yake ni kuhakikisha nyota hao wanazidi kuimarika na kurudi kwenye kasi yao.

**Suarez alifunga mabao mawili kwa Barca wakati ikitoka nyuma na kupata ushindi dhidi ya Inter kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita, huku Messi, ambaye alianza msimu huu kwa majeruhi akitengeneza bao la pili na kumaliza mchezo kwa dakika zote 90 msimu huu.**

Barca ilianza vibaya kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, kutokana na washambuliaji wake wote kukumbwa na majeraha, huku kikosi hicho cha Valverde kikiwa kimepitwa pointi tano na vinara Real Madrid na jana Jumapili walikuwa wanacheza na Sevilla.

Huku wote si Messi wala Suarez hawataichezea Argentina au Uruguay kwenye mechi za kimataifa zinazokuja, Valverde anajua kwamba kubaki kwako kwenye klabu kutawapa nafasi ya kuendelea kujiimarisha.

"Bila shaka wapo fiti tena, walionyesha hivyo (dhidi ya Inter)," alisema Valverde wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea mchezo wa jana Jumapili dhidi ya Sevilla pale Camp Nou.

"Nitaamua Jumapili (jana) kama wataanza wote au nitamwanzisha mmoja baadaye. Ni wachezaji wawili waliokuwa wanakabiliwa na majeraha msimu huu, lakini kwa jinsi wanavyocheza ndivyo wanavyopata nafasi ya kuwa fiti.

"Tungependa wachezaji wakazichezee nchi zao kwenye mechi za kimataifa, lakini tu kama wakiwa fiti, ila sasa watakuwa na nafasi ya kucheza hapa wakiwa wamebakia klabuni.

"Hakuna wachezaji wetu wengi ambao wanakwenda kwenye mapumziko ya mechi za kimataifa, lakini hilo ni jambo zuri kwetu.

"Hii inamaanisha kwamba tutakuwa na kikosi kamili kwenye mazoezi na kufanyia kazi vitu fulani.

"Na hiyo itakuwa muhimu kwa mechi zetu zinazokuja za La Liga na Ligi ya Mabingwa Ulaya na tunatakiwa kuwa tayari kwa yote.

"Tunafanya vizuri. Tutakuwa na wakati mzuri, sasa tunacheza kama timu imara zaidi, malengo yetu ni kuendelea kwenda mbele."

Barca imekuwa bila Jordi Alba tangu beki huyo wa kushoto alipoumia misuli ya nyama za paja kwenye sare na Borussia Dortmund mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya uliopigwa Septemba 17, lakini Valverde alithibitisha kwamba, nyota huyo wa timu ya Taifa ya Hispania, amerejea.

"Beki wetu wa kushoto sasa amepona na yuko fiti," alisema Valverde.

## ZISIKUPITE

### WENGER KUIBUKIA FIFA

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger anafikiria kuchukua madaraka ya ukurugenzi wa ufundi wa Fifa, lakini Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 68- hawezi kuweka kando kurudi kuwa kocha. ***(beIN Sports)***

### LUIZ AMFUNGUKIA LAMPARD

BEKI David Luiz, amesema "hakufikiria mara mbili" kuhusu kujiunga na Arsenal akitokea Chelsea majira ya joto, kwa sababu alikuwa na "mawazo tofauti ya mustakabali wa baadaye wa mchezo" na Frank Lampard. ***(Metro)***

### GUARDIOLA ATOSA MAKINDA

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema presha ya kushinda makombe inamfanya kuwa na wakati mgumu kutoa nafasi kwa wachezaji makinda. ***(Sunday Telegraph)***

### DE GEA KUINUNUA ELCHE

KIPA wa Manchester United, David de Gea, 28, yupo tayari kuinunua klabu ya Hispania, Elche kwa kulipa pauni milioni 16 wakati mpango huo ukiendelea. ***(Sport)***

### CHILWELL KUSEPA LEICESTER

LEICESTER City inasaka mbadala wa beki wa kushoto, Ben Chilwell, 22, wakati huu Chelsea na Manchester City zikiongoza mbio za kumwania nyota huyo wa kimataifa wa England. ***(Sun on Sunday)***

### UTD YAKANA MADAI POGBA

MANCHESTER United imekana madai kuwa kiungo Mfaransa Paul Pogba ametaka kulipwa pauni 600,000 kwa wiki ili kusaini mkataba mpya. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 26 mkataba wake hapo Old Trafford umebakiza miaka miwili kumalizika. ***(Sunday Mirror)***

### ARSENAL, MILAN KWA MALEN

ARSENAL itatoa changamoto kwa AC Milan katika mbio za kuinasa saini ya mshambuliaji wa PSV Eindhoven, Donyell , 20, na inaandaa kutoa ofa ya euro milioni 56 kwa Mholanzi huyo. ***(Tuttosport, via Calciomercato)***

### SON AITAMANI NAPOLI

WAKALA wa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na Korea Kusini, Son Heung-min, 27, amekataa kuweka kando uwezekano wa baadaye kujiunga na miamba ya Italia, Napoli. ***(Calciomercato)***

### AKERWA TETESI ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg, Erling Braut Haaland amesema tetesi za kuhusishwa na kujiunga na Arsenal na Manchester United "zinakera". ***(Football London)***

### LAMPARD AMSHUKIA PULISIC

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amemwambia winga Mmarekani, Christian Pulisic -pauni milioni 53 alizonunuliwa klabuni hapo akitokea Borussia Dortmund - hizo ni ada ya uhamisho tu na kwamba hazitoshi kumpa nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza. ***(Sunday Mirror)***

### WILSON AIVUTIA UNITED

MANCHESTER United inataka kumsajili straika Callum Wilson katika dirisha la usajili la Januari huku ikichombeza kumfanya apate nafasi ya kuitwa kikosi cha England kitakachoshiriki Euro 2020. ***(Sunday Express)***

HABARI MICHEZO

## Taifa Jang'ombe waiota Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya timu yake kupata pointi tatu muhimu, Kocha Mkuu wa Taifa Jang'ombe, inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, Suleiman Mohammed Suleiman "Mo", amesema ana matumaini makubwa kuwa timu hiyo itapanda Ligi Kuu.

Kocha huyo alisema maneno hayo baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Miembeni katika mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza uliochezwa juzi na goli hilo pekee lilipachikwa kwa penalti na Abdallah Munthir.

Alisema amekiandaa vema kikosi chake hicho chenye pointi sita, kuhakikisha kinashinda kila mchezo ili malengo yao ya kurejea Ligi Kuu Zanzibar yaweze kutimia.

"Tumesajili wachezaji wazuri na wazoefu, sioni sababu ya kutopanda daraja msimu huu, nina nyota wenye viwango vya kuipandisha timu hii, baada ya kuwafahamu vema wapinzani wetu," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Miembeni, Suleiman Mohmoud Jabir, alisema mchezo huo ulikuwa mgumu, lakini kupoteza mechi hiyo haimaanishi kikosi chake ni dhaifu.

Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inashirikisha timu 13 ambazo ni Taifa Jang'ombe, Miembeni, Mundu, Uhamiaji, Kikwajuni, Kilimani City, Idumu, Bweleo, Dulla Boys, Ngome, Mchangani United, Black Sailor na Mwembe Makumbi .

## Nikitas ajitosa uongozi MRFA

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Morogoro (MRFA), Aristotles Nikitas, amechukua fomu ya kuwania nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika ifikapo Oktoba 22, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nikitas, alisema baada ya kukaa nje ya uongozi kwa vipindi viwili, ameshawishika kurejea MRFA ili kuhakikisha anatoa mchango wa kuisaidia Morogoro iweze kusonga mbele katika mchezo huo.

Nikitas alisema muda wa kufanya kampeni utakapofika, ataelezea vema mipango yake ambayo anaamini itakuwa na matokeo chanya kwa mkoa wao.

"Nimechukua fomu ya kuwania nafasi ya Makamu Mwenyekiti, nimeona sitakuwa natenda haki kwa kukaa pembeni, wakati mimi ni Mwana-Morogoro halisi," alisema kwa kifupi mgombea huyo.

Morogoro unakuwa mkoa wa kwanza kufanya uchaguzi mkuu ambao unatarajia kutoa viongozi watakaokaa madarakani kwa muda wa miaka mingine minne na vile vile wataingia katika Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Katibu wa Kamati ya Uchaguzi ya MRFA, Roman Luoga, alitangaza juzi ndio ilikuwa siku ya mwisho kuchukua na kurudisha fomu za kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika chama hicho.

# KATWILA AFUNGUKA SIRI KUTWAA UBINGWA U-20

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa timu ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (U-20) ya Tanzania Bara, Zuberi Katwila, amesema haikuwa kazi rahisi kwa kikosi chake kutwaa ubingwa wa michuano ya Cecafa U-20 mbele ya wapinzani wao yosso kutoka Kenya.

Tanzania Bara ilitwaa ubingwa wa michuano hiyo juzi kwa kupata ushindi wa bao 1-0, baada ya mchezaji wa Kenya, Jackson Otieno kujifunga katika harakati za kuokoa hatari kwenye lango lao, sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila, alisema walitumia nguvu na akili nyingi kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika mchezo huo wa fainali na amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana wakati wote.

**Katwila alisema pia wachezaji wake walicheza kwa utulivu zaidi baada ya kuwasoma Kenya ambao walitoka nao sare ya mabao 2-2 katika mchezo wa hatua ya makundi.**

"Haikuwa kazi rahisi, mechi ilikuwa ngumu sana, tulijua itakuwa na changamoto kwa sababu kila mmoja anamjua mwenzake baada ya kukutana hatua ya makundi, tumepambana kwa kiasi kikubwa kuhakikisha tunashinda mchezo huu, utulivu pia ulitusaidia kupata ushindi," alisema Katwila.

Mshambuliaji wa timu hiyo, Kelvin Nashon, alisema kufuata vizuri maelekezo ya benchi lao la ufundi ndiyo siri ya wao kuibuka mabingwa wa mashindano hayo yaliyoshirikisha nchi 11 za Afrika Mashariki na Kati.

"Tulijiandaa vizuri, tuliifanyia sana mazoezi mechi hii ya fainali, kabla ya mchezo tulijifua sana na kujipanga imara, tulijua ubora na ugumu wa Kenya, tunamshukuru Mungu kwa kufanikiwa kushinda, tunafuraha sana," alisema Nashon.

Mbali na kutwaa ubingwa, pia mshambuliaji wa Tanzania Bara, Kelvin John, alitangazwa kuwa Mchezaji Bora na Mfungaji Bora wa michuano hiyo.

Kikosi hicho cha Tanzania Bara kilirejea nchini jana mchana.



Mkuu wa Huduma kwa Wateja wa MultiChoice Tanzania, Ngwitika Mwakihesya, akimwelekeza mmoja wa wateja waliofika katika tawi la MultiChoice Mlimani City, Aziz Makupa, jinsi ya kupata huduma mbalimbali za DStv ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. Kulia ni Ofisa wa Huduma kwa Wateja wa tawi hilo, Vedastina Ishengoma. Katika maadhimisho hayo, MultiChoice itatoa zawadi mbalimbali kwa wafanyakazi na wateja wake. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Wateja MultiChoice kuzawadiwa wiki yao*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya MultiChoice Tanzania, imeanza maadhimisho ya Wiki ya Wateja ambapo itaendesha shughuli mbalimbali ikiwamo kutoa zawadi kwa wafanyakazi na wateja kwa muda wa mwezi mzima.

Mkuu wa huduma kwa wateja, Ngwitika Mwakihesya, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, alisema katika kipindi hicho, MultiChoice Tanzania itakuwa na matukio mbalimbali yenye lengo la kuiwezesha kuwasogelea wateja karibu zaidi na kufahamu kwa kina uzoefu wao wa kupata huduma za DStv.

"MultiChoice inaamini kuwa wafanyakazi na wateja wetu ndiyo nguzo ya ustawi wetu hivyo katika kipindi hiki tutahakikisha tunawafikia na kuwasikiliza maoni yao na hili tunalifanya ili tuweze kuboresha zaidi huduma zetu na kumfanya mteja ajisikie kuwa yeye kweli ni mfalme," alisema Ngwitika na kuongeza kuwa mchakato huo utahusisha kuwazawadia wafanyakazi mbalimbali pamoja na wateja na pia kuwatembelea wateja wao maeneo mbalimbali ili kuwasikiliza na kupata maoni yao.

Aidha, amesisitiza kuwa kutokana na uzito huo, zoezi la kutembelea wateja litafanywa kwa kushirikiana na uongozi wa kampuni hiyo.

"Zoezi hili la kuwatembelea wateja litafanywa kwa kushirikiana na viongozi, hivyo hata mkurugenzi mwenyewe na timu yake ya menejimenti wataenda kuwatembelea wateja," alisisitiza Ngwitika.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 7, 2019

Nipashe




‘Uhusiano wa Neymar, mashabiki PSG’ UKURASA 28

KITU HICHO...



David Luiz akiifungia Arsenal bao pekee dhidi ya Bournemouth kwa kuunganisha kimyani kwa kichwa mpira wa kona uliochongwa na Nicolas Pepe kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates jana na wenyeji hao kushinda kwa bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yaanza Ligi

## ●●● Bao la Makame lazua utata, huku wachezaji wa Coastal Union wakiamini mpira ulikuwa...

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE Yanga imeandika ushindi wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu Bara msimu huu baada ya jana kuibanjua Coastal Union ya Tanga kwa bao 1-0 katika mchezo uliokuwa wa kushambuliana kwa zamu uliopigwa Uwanja wa Uhuru.

**Abdulaziz Makame ndiye aliyeiandikia Yanga bao hilo pekee ambalo lilizua utata kwa mashabiki na wachezaji wa Coastal wakiamini kwamba mpira ulikuwa haujavuka mstari wakati beki wa ‘Wagosi’ hao akiwa anaokoa.**

Bao hilo la dakika ya 51, lilipatikana baada ya Makame kuitendea haki pasi ya Ali Ali aliyepokea mpira wa kona kutoka kwa Mrisho Ngasa, hivyo kuifanya timu yake sasa kufikisha pointi nne baada ya kushuka dimbani mara tatu msimu huu.

Katika mechi hiyo ambayo, Yanga ilitawala kipindi cha kwanza, ingeweza kuanza kuandika bao katika dakika ya 10 kupitia kwa mshambuliaji David Molinga ‘Falcao’ lakini kichwa chake hakikuwa makini kulenga goli.

Dakika ya 28, kama Danny Lyanga angetulia mambo yangeweza kuwa mengine kwa upande wa Coastal Union, lakini akiwa peke yake na kipa wa Yanga, Farouk Shikhalo alipiga shuti fyongo ambalo alionekana kama vile kumpasia mlinda mlango huyo.

Juma Abdul nusura naye aihakikishie Yanga inakwenda mapumziko ikiwa kifua mbele, lakini shuti lake lilienda nje dakika ya 43 kabla ya dakika moja baadaye Feisal Salum ‘Feitoto’ shuti lake akipokea pasi kutoka kwa Molinga kukosa macho.

Kipindi cha pili baada ya Yanga kupata bao hilo, ilirudi nyuma kujilinda zaidi na kuwafanya kuruhusu mashambulizi lakini safu ya ushambuliaji ya Coastal Union haikuwa makini kuweza kuzitendea haki nafasi walizokuwa wakizitengeneza.

Coastal Union, ilifanya mabadiliko dakika ya 56 kwa kumtoa Hamis Kigundulu na nafasi yake kuchukuliwa na Haji Gando, huku dakika 13 baadaye Yanga ikimtoa Deus Kaseke na kumwingiza Jaffary Mohamed.

Kelvin Yondani alitoka kutokana na kupata majeraha dakika ya 77 na nafasi yake kuchukuliwa na Mharami Issa ‘Marcelo’, mabadiliko ambayo hayakuweza kubadili lolote kwa timu zote mbili na Yanga kuonekana kunufaika zaidi.

Dakika ya 81 Molinga alipachika bao, lakini tayari kibendera cha mwamuzi wa akiba kilishakuwa juu kuonyesha kwamba alikuwa ameotea.

Kwa matokeo hayo, Yanga ambayo ilikuwa na pointi moja iliyoipata baada ya Alhamisi kutoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Polisi Tanzania, huku ikiwa imegongwa mechi yake ya kwanza dhidi ya Ruvu Shooting, imefikisha alama nne kwenye ligi hiyo ambayo vinara ni mabingwa watetezi, Simba wakiwa na pointi 12 kufuatia kushuka dimbani mara nne.

Ligi hiyo sasa inasimama kupisha Kalenda ya Fifa ambapo wachezaji walioitwa kikosi cha timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars wataingia kambini leo kujiwinda mechi ya kirafiki dhidi ya Rwanda kabla ya kwenda Sudan kuvaana na Wasudan hao kwenye mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Afcon kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) Oktoba 18, mwaka huu.


# Miraji atoa siri ya tuzo Simba SC

**Na Somoe Ng’itu**

MSHAMBULIAJI wa Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Miraji Athumani, amesema amerudi katika klabu hiyo ili aweze kutimiza ndoto zake za kufika mbali katika mchezo huo unaopendwa na watu wengi duniani.

Miraji maarufu kama ‘Shevchenko’, wengi wakimwita kwa kifupi “Sheva”, kama wenzake wanavyomwita tangu akiwa Simba B, amesema hayo baada ya kuchaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mwezi Septemba mwaka huu.

Mshambuliaji huyo aliyerejea Simba akitokea Lipuli FC, amefunga mabao mawili kati ya 10 ambayo yamefungwa na mabingwa hao watetezi kwenye mechi nne walizocheza msimu huu.



Akizungumza na gazeti hili jana, Miraji, alisema kuwa kila atakapopata nafasi ya kucheza, atakuwa anajituma kwa sababu mawakala na makocha mbalimbali wa kigeni wanaangalia zaidi Simba kuliko timu nyingine inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Miraji alisema pia anashukuru ushirikiano na umoja anaoupata katika kikosi cha Simba na anaamini hali hiyo ikiendelea, ataifanyia makubwa zaidi.

“Namshukuru Mungu nimepata tuzo ya kwanza ya Ligi Kuu, ni tuzo ambayo kila mchezaji amekuwa na ndoto nayo, lakini ushirikiano kutoka kwa wachezaji wenzangu ndio umenifikisha hapa nilipo, naamini nitafanya mengi zaidi katika mechi zinazokuja,” alisema Miraji.

Mbali na Miraji, Kocha Mkuu wa Simba Mbelgiji Patrick Aussems naye alichaguliwa kuwa Kocha Bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara Septemba, kwa kutwaa tuzo hizo, kila mmoja atapata zawadi ya Sh. milioni moja kutoka kwa wadhamini wa tuzo hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002